SportPesa
TZS. 823,998,440
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Shahidi** atoa sababu Sabaya kushikiliwa zaidi ya saa 48

UKURASA 3



**Dest kumrithi Trippier Atletico Madrid**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumamosi Januari 8, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580819

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Maonyo mazito ya Samia vijana wa CCM

• **Awataka** waache kuwa madaraja, kutokuwa chanzo mpasuko ndani ya chama...*Uk.2*



Mwenyekiti CCM Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea bendera ya Zanzibar kutoka kwa Rajab Ali Rajab, kwenye maadhimisho ya Kilele cha Matembezi ya miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Uwanja wa Makombeni, Wilaya ya Mkoani, Kusini Pemba jana. **PICHA: IKULU**

## Aliyedaiwa kumuua mke na kukimbia mbaroni

UKURASA 3



Job Ndugai




James Mbatia

## NCCR Mageuzi yatishia kupinga kortini kujiuzulu kwa Ndugai

UKURASA 2

MICHEZO YANGA PRINCESS YAIPANIA SIMBA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6



Mwenyekiti wa Chama cha NCCR- Mageuzi Taifa, James Mbatia akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuhusu kujiuzulu kwa Spika Job Ndugai akidai kuwa haitambuliki kisheria. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Maonyo mazito ya Rais kwa vijana wa CCM

**Na Mary Geofrey**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameutaka Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), kujiepusha na rushwa na kugeuzwa kuwa madaraja ya kuvusha watu kwenye uchaguzi wa ndani ya chama hicho.

Sambamba na hilo, wametakiwa kutokuwa chanzo cha mpasuko ndani ya chama badala yake wasimame na kukitetea kwa maendeleo ya chama na taifa kwa ujumla.

Rais Samia Suluhu Hassan alitoa rai hiyo jana katika Maadhimisho ya Kilele cha Matembezi ya Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar, yaliyofanyika Kusini Pemba.

"Mmezungumza suala la uchaguzi wa mwaka huu na hapa ndipo nawataka msifanye zilongwa mbali zitendwa mbali (yanayosemwa ni tofauti ya yanayotendwa). Uzoefu unaonyesha kwamba vijana mnageuzwa ngazi sana, mnadanganywa na vifedha kidogo na vinafasi. Mnainamishwa migongo, watu wanapanda juu ya migongo yenu. Wakishapata wanayotaka hawana habari na nyie.

"Kama wote mnaowabeba wangefanya kazi 'ki haki lilah' kuwafanyia vijana, changamoto nyingi tunazozungumza leo zisingekuwapo," alisema na kubainisha kuwa uchaguzi ndani ya jumuiya hiyo, unasimamiwa kwa mujibu wa kanuni na miongozo, hivyo wote wanatakiwa kuwania nafasi hizo.

"Vijana mna haki zote za kuchagua na kuchaguliwa, nendeni mkagombee. Mimi nawahakikishia zitakapokuja juu kwetu hatutazama sura, tutatazama uwezo, tutatazama weledi na uwezo, kwa maana hiyo nendeni mkagombee," alisisitiza.

**CHANZO MPASUKO**

Rais Samia pia aliwataka vijana wa CCM kutokutoa fursa wala kutumika kutengeneza mpasuko ndani ya chama.

"Msitoe fursa ya kutumika kukipasua chama. Jeuri yenu, kujidai kwenu na kutembea kifua mbele ni kwa sababu chama kipo imara. Mtakapokipasua vipande vipande, hamtayafanya haya mliyoyafanya leo," alisema Samia.

"Kwa hiyo nawaombeni sana nendeni mkaimarishe chama chenu. Kaimarisheni jumuiya yenu, kaimarisheni chama chenu, vijana msitumike vibaya," aliongeza.

Rais Samia alisema ukombozi wa kisiasa ulishafanyika na vijana wa zamani, vijana wakasomeshwa ili kusimama wenyewe ambao ndiyo viongozi wa sasa, hivyo akawataka vijana kutambua kuwa, mapinduzi yaliyobaki ni ya maendeleo ya kunawirisha na kustawisha taifa.

Aliwasishi vijana hao kusimamia hilo na kuchangamkia fursa zinazotolewa na serikali katika kukuza uchumi wa taifa na pia kwenda kuchambua risala yao waliyomsomea, kujua ni mambo yapi wameyafanyia kazi na yapi ambayo hawajayafanyia kazi bali waliyazungumza kwa ajili ya mkutano huo tu.

"Mjue yapi mmefanya na yapi hamjafanya na mtafanya kwa mikakati ipi na mnakwenda kusimamaje halafu mtuleee tuwasaidie," alisisitiza na kuwataka vijana kutumia fursa zilizopo nchini kwa kutembelea vyuo vya ufundi stadi kujifunza namna ya kujiajiri na kukuza vipato vyao.

**UNYANYASAJI KIJINSIA**

Kadhalika, Rais Samia alisema katika uchaguzi ndani ya UVCCM kuna tawala fitina, rushwa na mambo kadhaa na kwamba ukifika muda huo, wenye watoto wa kike wanakuwa roho juu kuhofia usalama wao kutokana na kutawala kwa rushwa ya ngono.

"Kwenye risala yenu hapa mmesema mnaenda kupinga matendo yote ya unyanyasaji na udhalilishaji wa kijinsia katika uchaguzi huo. Naomba mkasimame. Mwanamke ni kijana, mwanamke ni mama wote wana uwezo sawa, acheni kunyanyasa dada zenu, acheni kudhalilisha ndugu zenu," alisema Samia.

Alisema anayesimama kuwania akiwa na sifa apewe nafasi ya uongozi na kuwataka kuondokana na mazoea yasiyofaa katika uchaguzi huo.

**AHIMIZA CHANJO**

Rais Samia pia aliwataka vijana kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 ili kuepuka kupata maambukizi na hatari ya kuugua.

"Msigeuke kauli ya Wandengereko inayosema zilongwa mbali, zitendwa mbali. Maana yake kwenye risala maneno ni mazuri sana lakini kwenye uhalisia sina uhakika. Nawaombeni vijana mkachanje, chanjo ni bure, chanjo zipo, ukichanja sikuhakikishii hutapata Uviko-19. Unaweza kupata lakini ukaendelea na shughuli zako," alisema.

**TATIZO LA AJIRA**

Alisema pamoja na mambo mengine anatambua kuwapo kwa tatizo la vijana wengi kukosa ajira na mitaji ya kujiajiri na kujipatia kipato.

"Hilo tunalitambua na tunatambua upungufu wa ajira ni wa nchi nzima na popote duniani mabadiliko yanapotokea tatizo hili linazidi kuwa kubwa zaidi. "Tumekumbwa na balaa la UVIKO-19 viwanda vingi vimefungwa na waliokumbwa na punguzo la wafanyakazi ni vijana," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali inajitahidi kutengeneza ajira kupitia nyanja tofauti, ajira ndani ya serikali, vikosi vya ulizi na miradi ya serikali inayoendelea.

"Takwimu za ajira zinapaa kufikia 14,000 hivyo serikali inaendelea kujitahidi kutengenea fursa mbalimbali ili vijana wapate ajira," alisema Rais Samia.

Kuhusu mabadiliko ya tabia nchi, Rais Samia alisema ni changamoto iliyopo duniani kote, lakini ni fursa kwao vijana endapo wakijiunga na kujifunza namna ya kukabiliana nayo.

Alisema ni eneo la vijana kuchangamkia kwa sababu linaathiri zaidi kina cha bahari kutokana na kuongezeka kwa joto hasa kwa Zanzibar.

Rais Samia alisema bahari inaendelea kuingilia maeneo ya watu na visiwa vinazama kwa sababu bahari inakuja juu tofauti na awali ilikuwa chini zaidi.

"Nitoe wito kwa viongozi wa ngazi zote pamoja na vijana kutumia fursa zinazojitokeza katika maeneo mbalimbali," alisema Rais Samia.

# NCCR yatishia kupinga kortini kujiuzulu Ndugai

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha NCCR-Mageuzi kimetishia kwenda mahakamani kupinga kujiuzulu kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kwa madai kwamba hakufuata utaratibu wa kikatiba.

Wakati chama hicho kikikusudia kufanya hivyo, hatua ya kujiuzulu kwa Ndugai imesababisha kamati za kudumu za bunge kushindwa kuanza kazi kama ilivyopangwa kutokana na kuwapo kwa ombwe la nafasi ya Spika.

Mwenyekiti wa NCCR Mageuzi, James Mbatia, alisema jana Dar es Salaam kwamba kitu kilichofanyika juzi hekima na busara havikutumika wala si kikatiba, kisheria na kimantiki hivyo mpaka sasa wanamtambua Ndugai kwamba bado ni spika wa bunge.

"Katiba hii tuliyo nayo tuiheshimu kwanza sheria tulizo nazo tuziheshimu, tuache kuwa juu ya Katiba. Tunajua tuna mgogoro wa kikatiba, tuheshimu lakini tuharakishe mchakato ili kuondokana na hii migogoro na taifa listawi," alisema.

Mbatia alisema mihimili mitatu iliyopo nchini inategemeana kwa misingi ya kustawisha na kuifanya jamii iwe katika hali nzuri na si kwamba mhimili mmoja kuwa na mamlaka ya kuongoza au kuingilia mwingine.

Alisema tukio la kiongozi mkuu wa mhimili wa dola kujiuzulu nafasi yake, lina uzito unaoendana na tukio la kiongozi huyo kuchukua nafasi hiyo na kwamba kitendo cha kiongozi huyo kuwasilisha barua ya kujiuzulu kwa Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ni kinyume cha Katiba.

"Utaratibu wa namna ya spika kujiuzulu uko kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 149 inayosema: "Iwapo mtu huyu ni Spika au Naibu Spika wa bunge basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwenye bunge.

"Ndugu zangu chonde chonde tutakosa control (udhibiti). Migongano inayoendelea isiposimamiwa vizuri, taifa letu tutaangamia na sisi hatutaki tuangamie. Tuko tayari kushauri, kujadiliana na kuweka uongozi,' alisema.

Pia alitoa rai kwa viongozi wastaafu wakiwemo marais, majaji na viongozi wa dini kusimama vizuri kwa kushauri taifa vizuri na kuzungumza kwa maslahi ya taifa.

**KAMATI ZASIMAMA**

SIKU moja baada ya Ndugai kujiuzulu, Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, ametangaza kuahirishwa kwa vikao vya kamati za bunge ambavyo vilipangwa kuanza wiki ijayo.

Pia amesema taratibu za kujaza nafasi hiyo ya kiti cha Spika ambayo iko wazi kwa sasa zinaendelea.

Kwa mujibu wa tangazo la Katibu huyo, lililotolewa jana kwa wabunge, hakuna shughuli zitakazoendelea kwa kipindi ambacho nafasi ya Spika iko wazi, hivyo aliwaagiza wabunge wote kufika Dodoma Januari 31, kwa ajili ya kuanza Mkutano wa Sita wa Bunge utakaoanza Februari Mosi.

Taarifa hiyo ilisema: "Kamati za Bunge zilizokuwa zikutane Januari 10 na 17 mwaka huu hazikutani tena katika kipindi hicho na badala yake zitakutana wakati wa mkutano wa sita wa bunge Februari Mosi, 2022."

Mwihambi alisema kutokana na kujiuzulu kwa Spika wa Bunge, kamati za kudumu zilizokuwa zikutane kuanzia Januari 10, mwaka huu, na zilizotakiwa kukutana Januari 17 hazitakutana kwa wakati huo tena.

"Kwa mujibu wa ibara ya 84(1) ya Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977, Spika ndiye kiongozi wa Bunge na ndiye msimamizi wa shughuli zote za bunge.

"Ibara ya 84 (8) inaelekeza kwamba kiti cha Spika kinapokuwa wazi hakuna shughuli yoyote itakayotekelezwa katika Bunge isipokuwa uchaguzi wa Spika,"ilieleza sehemu ya taarifa hiyo.

Juzi, Ndugai aliandika barua kwa Katibu Mkuu wa (CCM) kwa Mwenyekiti wa CCM na nakala yake kwenda kwa kwa Katibu wa Bunge akieleza nia yake ya kujiuzulu nafasi hiyo.

Kujiuzulu kwa Spika Ndugai kulitokana na kauli yake aliyoitoa Desemba 26, mwaka jana iliyoonekana kupingana na serikali ya awamu ya sita kukopa mikopo.

HABARI KITAIFA

## Aliyedaiwa kuua mke, kisha kukimbia akamatwa

**Na Maulid Mmbaga**

JESHI la Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam linamshikilia Isaya Mnzava (59), mkazi wa Bunju Beach, Dar es Salaam, kwa tuhuma za kumshambulia na kumuua kwa kutumia kitu chenye ncha kali mke wake, Irene Mnzava (56).

Kamanda wa Kanda hiyo, Jumanne Muliro, alisema hayo jijini Dar es Salaam jana kuwa Irene alikuwa mfanyakazi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na aliuawa na mume wake Desemba 26, mwaka jana, majira ya saa 6:00 usiku maeneo ya Bunju.

Alisema baada ya mtuhumiwa kutekeleza mauaji hayo, alitoroka na kwenda mkoani Kilimanjaro kwa kutumia gari lenye namba za usajili T 727 DKK Toyota Harrier na alipobaini anafuatiliwa, alilitelekeza gari hilo Moshi mjini na kwenda Arusha.

"Jeshi la Polisi liliendelea kumfuatilia ambapo alikimbilia mkoa wa Shinyanga, wilayani Kahama. Ufuatiliaji wa kina ulipofanyika, ilibainika kwamba alikimbia tena na kwenda mkoa wa Kagera, wilayani Muleba.

"Januari 4, mwaka huu, mtuhumiwa alikamatwa katika kijiji cha Kagoma wilayani Muleba, kurudishwa Dar es Salaam," alisema Muliro.

Aliongeza kuwa kilichofanywa na mtuhumiwa huyo ni kitendo cha kikatili ambacho hakivumiliki ndiyo maana Jeshi la Polisi lilifanya kila jitihada kuhakikisha anakamatwa na kufikishwa mahakamani ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

Muliro aliwataka wananchi kujiepusha kufanya matukio ya kihalifu kwa kufikiri kuwa wanaweza kukimbia na wasipatikane kwa kuwa yeyote atakayejihusisha na vitendo hivyo, atafuatiliwa na sheria kali itachukuliwa dhidi yake.

"Jeshi la Polisi Kanda Maalumu linasisitiza ukifanya tukio la kihalifu litakufuatilia mahali popote ulipo iwe ndani au nje ya Mkoa wa Dar es Salaam na utakamatwa na kurejeshwa kwenye eneo ulikofanya tukio kwa hatua zaidi za kisheria," alisema Muliro.

# Shahidi atoa sababu kumshikilia Sabaya mahabusi zaidi ya saa 48

**Na Allan Isack,** ARUSHA

JUMA Ramadhani, shahidi wa 13 wa Jamhuri katika kesi ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amedai kuwashikilia mshtakiwa huyo na wenzake kwa zaidi ya saa 48 kutokana na tuhuma nyingi zilizokuwa zinawakabili.

Shahidi huyo, ambaye ni Ofisa Uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), alitoa madai hayo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha mbele ya Hakimu Mkazi, Patricia Kisinda, wakati akihojiwa na wakili wa utetezi, Sylvester Kahunduka.

Katika shauri hilo namba 27 la uhujumu uchumi, mbali na Sabaya, washtakiwa wengine katika shauri hilo ni Sylvester Nyengu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Ramadhani alidai kuwa waliwashikilia washtakiwa hao kwa siku sita kwa kuwa walikuwa wanakabiliwa na tuhuma nyingi, hivyo walipaswa kufanya uchunguzi wa kina ili kuthibitisha.

Alidai kuwa katika uchunguzi wake, alikuwa akipata taarifa nyingi fiche ambazo alizifanyia uchunguzi ili kuthibitisha kama ni za kweli na kwamba taarifa hizo zilimsaidia katika uchunguzi wake, kubaini na kuthibitisha matukio ya uhalifu aliyofanya na washtakiwa hao.

Shahidi alidai Januari 22, 2021, Sabaya alikutana na vijana wake katika hoteli ya Point Zone kuunda kundi la kutenda uhalifu na ili kuthibitisha kuwa hilo ni kweli, alijiridhisha kwa kufanya mahojiano ya awali na washtakiwa, wakiwamo John Odemba na Nathan Msuya.

Alidai kuwa kwa mujibu wa taarifa za kampuni za mawasiliano, siku hiyo, Sabaya na vijana wake walitoka Hai na kwenda Arusha kwa ajili ya kutenda uhalifu na kwamba katika operesheni ya kumkamata Sabaya na vijana wake, walikamata simu zaidi ya tano.

Juma alidai kuwa Sabaya alikamatwa jijini Dar es Salaam Mei 27, 2021 na alichukuliwa maelezo ya onyo siku alipokamatwa na kufikishwa mahakamani Juni 4, mwaka jana.

Pia alidai kwamba Agosti 18, mwaka jana, alikwenda Magereza kuwahoji washtakiwa hao, akiwamo Sabaya lakini hakufanikiwa kuchukua maelezo yake kwa kuwa alidai hawezi kuhojiwa pasipo kuwapo wakili wake.

Alidai kuwa alikuwa na kibali cha mahakama kwenda Magereza kwa kuwa vitu ambayo alitaka kumhoji havihusiani na kesi inayoendelea mahakamani bali ni tuhuma zingine zinazomkabili.

Vile vile alidai alithibitisha tuhuma zinazowakabili washtakiwa kwa kuwahoji na kuchukua maelezo ya awali bila ya kuwashurutisha.

Kuhusu gari, shahidi huyo alidai kwamba walifikisha mahakamani kama kielelezo cha ushahidi kwa kuwa fedha zilizotumika kununua zimetokana na zao la rushwa.

Alidai siku 10 baada ya fedha hizo kuchukuliwa kwa mfanyabiashara Francis Mroso, zilitumika kununua gari aina ya Toyota Landcruiser T222DBY VX V8 na kwamba Sabaya alitumia fedha za rushwa Sh. milioni 90 kununua gari hilo.

"Baada ya Sabaya kuchukua fedha hizo za rushwa kutoka kwa Mroso, alitoa mgawo kwa vijana wake na kunywa, kula na kulala katika hoteli ya Tulia Lodge," alidai na kuongeza kuwa wakati wakimkamata Sabaya Dar es Salaam, alikuwa na fedha ambazo zitatumiwa kama kielelezo cha ushahidi kwenye kesi zingine zinazomkabili.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako akizungumza wakati wa uzinduzi wa Baraza la saba la Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Elimu Tanzania, Maulid Mwatala. PICHA: JUMANNE JUMA

# Waziri apiga marufuku upimaji ardhi mabondeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, imezipiga marufuku halmashauri nchini kupima viwanja na kumilikisha watu katika maeneo ya mabondeni na yale hatarishi.

Waziri wa wizara hiyo, William Lukuvi, alipiga marufuku hiyo jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu uzinduzi wa kituo cha mawasiliano kwa umma cha wizara hiyo.

Lukuvi alisema kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi, ni marufuku kwa mamlaka yoyote kupima na kumilikisha viwanja katika maeneo ya mabondeni na yale ambayo ni hatarishi.

"Ni marufuku kwa mamlaka yoyote au mtu yeyote kupima au kumilikisha mtu kiwanja katika eneo la bonde au eneo hatarishi kwa yeyote atakayebainika kufanya hivyo tutakula naye sahani moja.

"Natoa onyo kwa mamlaka za upimaji ardhi kuacha kufanya ujanja ujanja wa kufanya upimaji wa viwanja katika maeneo hatarishi na mabondeni kama ipo haja ya maeneo hayo kupimwa basi yatapimwa kwa maelekezo maalumu," alisisitiza Lukuvi.

Akizungumzia uzinduzi wa kituo hicho alisema kwa kutumia maendeleo ya TEHAMA yaliyopo kwa sasa na kwa kuzingatia uchukuaji wa hatua stahiki za kujikinga na Uviko-19 wizara imeona kuwa zipo baadhi ya huduma za ardhi zinazoweza kutolewa kwa njia ya simu na mitandao ya kijamii ambazo hazimlazimu mwananchi kufika katika ofisi za ardhi.

"Wizara imeanzisha kituo cha mawasiliano kwa wateja kitakachotoa huduma ya mawasiliano moja kwa moja na mwananchi kwa kutumia simu na ujumbe wa maneno kupitia WhatsApp na kutoa majibu au ufafanuzi kwa wananchi hao." alisema

Alisema ni matumaini yake kuwa kituo hicho kitatoa fursa kwa wananchi kupata huduma za ardhi kwa haraka, kwa ufanisi na kwa gharama nafuu kwa kuwa mwananchi hatalazimika kufika katika ofisi za ardhi endapo huduma anayoihitaji anaweza kuipata kupitia simu.

Alisema bado zipo huduma nyingine zitakazomhitaji mwananchi kufika katika ofisi za ardhi ili aweze kuhudumiwa.

Alitoa rai kwa wananchi kukitumia kituo hicho kwa kupiga simu na kutuma ujumbe wa maneno kupitia namba ya simu iliyotangazwa na kutumia tovuti ya wizara kupata huduma kwa urahisi bila usumbufu.

# Shigela awatumia salamu wazazi wakaidi

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, ameonya kuwa hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mzazi atakayeshindwa kumpeleka mtoto shuleni kwa kuwa atakuwa anapingana na juhudi za ujenzi wa madarasa zilizofanywa na serikali.

Shigela alisema hayo jana akiwa kwenye shule shikizi ya msingi Koo, alipotembelea miradi ya ujenzi wa miundombinu ya afya na elimu chini ya mpango wa maendeleo kwa ustawi wa taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 kimkoa.

Alisema wako baadhi ya wazazi waliozoea kuwazuia watoto kwenda shuleni hasa wanaoingia kidato cha kwanza kwa sababu mbalimbali ikiwamo kuwaozesha na kuwafanya kitega uchumi kwa kuwafanyisha kazi za ndani kwenye majumba ya watu.

"Rais Samia Suluhu Hassan ametuletea fedha. Madarasa yapo ya kutosha na madawati yapo na elimu ni bure bila malipo. Nasisitiza mtoto asipokwenda shuleni lazima sheria zifuatwe kwa wakuu wa wilaya kupitia vyombo vya ulinzi na usalama kuwakamata wazazi na kuwafikisha kwenye vyombo vya sheria kwa sababu ya kumkosesha mtoto kupata elimu ambayo ni haki yake," alisema.

Pia alisema kutokana na fedha za UVIKO-19, kuna shule mpya za sekondari 23 na shule mpya za msingi 41 ambazo kutoka kuwa shule shikizi zitasajiliwa kuwa shule rasmi za msingi.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mikese ambayo ni shule mama ya shule shikizi ya msingi Koo, Geofrey Kiangi, alisema Shule ya Msingi Koo ina wanafunzi 158 wakifundishwa kuanzia elimu ya awali hadi msingi.

Alisema kuboreshwa na kuongezwa madarasa katika shule hiyo kutasaidia wanafunzi kuendelea kusoma hapo na kuepukana na adha ya kutembea umbali mrefu wa zaidi ya kilometa 10 kwenda na kurudi kutoka Mikese kufuata elimu.

Naye mwalimu wa kujitolea katika shule shikizi ya Koo, Petro Tumai, alimshukuru Rais Samia kwa kuhakikisha ujenzi wa madarasa mawili katika eneo lao unaenda sambamba na madawati ili kuwafanya wanafunzi kuepukana na adha ya kukaa chini.

Alisema akiwa mchungaji aliyefika eneo hilo kueneza injili aliamua kuanzisha shule hiyo mwaka 2014 huku ikiwa na darasa na haikuwa na dawati hata moja bali wanafunzi walikaa chini huku wakisoma na kilichotokea kwa sasa anaona kama ni ndoto shule zikifunguliwa pia na wanafunzi watashangaa.

Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Morogoro, Elias Mpanda, alipongeza juhudi na hekima za Rais Samia kwa kutoa fedha hizo ili kujenga madarasa na madawati kwa lengo la kupambana na UVIKO-19.

Alisema awali shule nyingi wanafunzi walikaa 55 hadi 65 katika darasa moja na kufanya msongamano madarasani lakini kwa sasa watakaa kwa nafasi na kutakuwa na hewa nzuri itakayowawezesha kusoma na kuwa na ufaulu mzuri.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ,William Lukuvi, akikata utepe kuzindua kituo cha mawasiliano kwa wateja cha wizara hiyo, katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mary Makondo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mbunge ahofia bandari kuwa makumbusho

**Na Abdallah Khamis,** MTWARA

MBUNGE wa Lulindi mkoani Mtwara, Issa Mchungahela, amehofia bandari ya Mtwara kugeuka eneo la makumbusho ya kitalii kama hakutakuwa na jitihada za kuitangaza na kufanya kazi kwa ufanisi.

Amesema licha ya serikali kufanya maboresho mbalimbali yaliyogharimu Sh. bilioni 150, bado bandari hiyo haionyeshi jitihada za kuwavutia watumiaji kwa ajili ya kufanya kazi kipindi chote cha mwaka.

Mchungahela alitoa kauli hiyo jana mkoani hapa wakati akichangia mada katika kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC) kilichowahusisha wadau wa mkoa huo.

Alisema hatua ya kwanza ya kuielekeza bandari hiyo kwenye makumbusho ya kitalii ni pale iliposhindwa kusafirisha shehena zote za korosho hadi ikaamuliwa baadhi ya shehena kusafirishwa kwa njia ya barabara kwenda Bandari ya Dar es Salaam.

"Bandari ni muhimu lakini tunavyoenda sasa inaweza kubaki kuwa sehemu ya makumbusho ya taifa ya watu kujionea eneo lisilofanya kazi ipasavyo licha ya kuwekwa fedha nyingi za maboresho ya miundombinu. Nashauri bandari itumie njia mbalimbali ya kuitangaza, ikibidi hata magari na bidhaa za nchi jirani zipitie hapa," alisema Mchungahela.

Mohamed Kalumuna aliyemwakilisha Kaimu Meneja wa Bandari ya Mtwara katika kikao hicho, alisema baada ya maboresho ya miundombinu ya Bandari ya Mtwara, kumefanyika jitihada mbalimbali za kuvutia wateja kwa ajili ya kutumia bandari hiyo kusafirisha bidhaa zao.

Alisema moja ya njia hizo ni pamoja na kushusha baadhi ya tozo, ikiwamo tozo ya uhifadhi wa mizigo (wharfage) ya asilimia 0.5 ya freight on board (FOB) kwa mazao yote ya kilimo yanayosafirishwa nje ya nchi zikiwamo korosho.

Kalumuna alitaja changamoto zingine katika bandari hiyo ni pamoja na kutosafirisha shehena zote za korosho ghafi kwenda masoko ya nje kama ilivyoelekezwa katika malengo.

Padri Patric Mwaya wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mtwara, alisema kutosafirisha korosho kupitia Bandari ya Mtwara kama ilivyofanywa mwaka huu ni dalili za wazi za kuhujumu juhudi na uchumi wa wakazi wa Mtwara.

# Akutwa kafa kwa kujinyonga gesti

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

JOHN Jackson anayekadiriwa kuwa na miaka kati ya 20 hadi 25, amekutwa amekufa kwa kujinyonga na shuka katika nyumba ya kulala wageni Amazon iliyopo jijini Arusha.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Arusha, Justine Masejo amethibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuelezea kuwa chanzo cha marehemu kujinyonga bado hakijajulikana kwa kuwa hakuacha ujumbe wowote wa maandishi.

Alisema mwili wa marehemu umehifadhiwa katika chumba cha maiti katika Hospitali ya Mkoa Mount Meru kwa ajili ya kuuchunguza zaidi na kusubiri ndugu wa marehemu kuja kuutambua mwili.

Kugundulika kwa mwili wa marehemu ni baada ya mhudumu wa nyumba hiyo ya kulala wageni aitwaye Eunice Mianga, kwenda kufanya usafi Januari 5, mwaka huu majira ya saa tano asubuhi alipokwenda kufanya usafi alipofika mlangoni aligonga mara kadhaa pasipo kufunguliwa.

Eunice alisema kuwa marehemu alifika katika nyumba hiyo, kama mteja wa kawaida na kuandikisha jina kwenye kitabu cha wageni, akidai anatokea jijini Mwanza akielekea wilayani Moshi, alipatiwa chumba namba 17.

Alisema baada ya kukabidhiwa chumba hicho muda mfupi baadaye mteja huyo alitoka nje na wakati anarudi alionekana akiwa amebeba chupa ya pombe kali aina ya K Vant na kupitiliza moja kwa moja chumbani kwake.

Mhudumu huyo alisema ilipofika Januari 6 majira ya saa tano asubuhi alienda kumgongea mlango marehemu ambaye hakuonyesha dalili za kufungua ndipo alipochungulia kupita upenyo wa dirisha na kuona shuka nyeupe ikiwa juu na marehemu akiwa ananing'ia kwenye dirisha.

Alisema: "Niliamua kumwita mlinzi na yeye kushuhudia tukio hilo na baadaye tulitoa taarifa Polisi, polisi walifika na kuvunja mlango na kuutoa mwili, lakini katika chumba hicho kulikuwa na chupa ya K-vant, chupa ya soda na dawa ambazo hazikujulikana".

**TANGAZO**

# TANZANIA WILDLIFE MANAGEMENT AUTHORITY

# INVITATION TO PARTICIPATE IN ELECTRONIC AUCTIONING

***(Made under regulation 8 of the Wildlife Conservation [Tourist Hunting] Regulations, 2015)***

Tanzania Wildlife Management Authority (TAWA) invites applications from qualified applicants for the allocation of Tourist Hunting Blocks through electronic auctioning (e-auctioning). Currently, there are 75 hunting Blocks within Game Reserves (GRs), Game Controlled Areas (GCAs) and Open Areas (OAs) that are immediately available for e-auctioning. The 75 hunting blocks are in two groups (A comprising 26 blocks which their tenure will commence immediately after the auctioning exercise in 2022 and B comprising 49 blocks which their tenure will commence on 1st January 2023). Eligible hunting companies can be allocated up to five (5) hunting blocks each, which shall be of different categories. **Auctioning will commence on 12th January 2022, and will last for seven consecutive days.**

**1. QUALIFICATIONS FOR ALLOCATION OF HUNTING BLOCK (S)**

According to the Wildlife Conservation Cap. 283, no person shall be considered for allocation of a hunting block unless:

(a) He has a company registered with the Registrar of Companies within Tanzania intending to engage in hunting of animals;
(b) At least one of the Directors has five (5) years experience in Wildlife based business and Conservation in Tanzania; and
(c) The company meets requirements of Section 39(3)(a) of the Wildlife Conservation Act.

**2. TENURE OF OWNERSHIP OF HUNTING BLOCKS**

The tenure of ownership of hunting blocks shall be **10 years for Category I and II** hunting blocks and **15 years for Category III** hunting blocks. The Minister shall on the fifth year of the tenure of ownership of a hunting block, determine the continuity of the tenure. The Minister's decision shall be based on:

a) the annual performance assessment and the evaluation of the hunting block utilization; and
b) the full performance of the company allocated a hunting block to be carried out in the fourth year of the tenure, which shall take into account the annual assessment and the evaluation criteria prescribed in the regulation.

**3. MODE OF APPLICATION AND INSTRUCTIONS**

a) Applicants will complete an online registration at **http://portal.maliasili.go.tz** through the appropriate e-form provided. After successful registration an applicant will be assigned an auto generated username and password sent via their registered e-mail addresses to enable them to access the e-auction portal,
b) Applicants will then select hunting blocks they intend to bid, which will automatically generate an e-invoice for the applicant to pay a non- refundable application fee based on the block category being applied for (see table below).

**Application fees per categories of hunting blocks**

Applicants **will pay a single application fee per category** (and apply across the category) **not per category per block.**

| S/N | Category of Hunting Block | Fees per category in USD |
|---|---|---|
| 1 | I | 5,000 |
| 2 | II | 2,000 |
| 3 | III | 1,000 |

c) Only applicants who paid registration fees will be permitted to participate in e-auctioning of hunting blocks, which will remain open for a period of seven consecutive days.
d) A bidder will use his/her username and password to access the bidding dashboard and bid according to the information specified on the bidding interface.
e) A bidder will remain anonymous.
f) Bids will be automatically ranked, the contents of which will be encrypted.

**Bidders will:**

g) Assign a fee and compete only on pre-selected hunting block(s),
h) Log in the e-auction system more than once during bidding,
i) Be notified automatically on new bids as they are placed, together with their corresponding prices, so that they will be able to track their rankings in the course of bidding,
j) Identities of bidders shall not be disclosed by any party during the course of auctioning,
k) All invalid bids submitted shall be rejected with a message explaining reasons for a rejection,
l) Bidders shall not provide any additional information or clarifications related to the auction that may distort competition; and where necessary, such information shall be availed by TAWA,
m) Users shall be responsible for maintaining the confidentiality of all particulars associated with their accounts,
n) An e-auction award shall be based solely on ranking of prices, such that the allocation is awarded to the highest successful bidder,
o) No bid may be withdrawn after the completion of bidding process,
p) Bidders will only be allowed to increase their bidding prices during the auctioning process,
q) A successful bidder shall pay 100% of the highest price reached within fourteen (14) days from the date of receipt of due diligence results, failure of which will lead into cancellation of the offer, and,
r) A successful bidder shall pay the hunting block fees annually equivalent to his bid price.

**NOTE:**
Only successful bidders will be issued with a Hunting Block Allocation Certificate by the Minister. Should you need any further information or clarifications, please do not hesitate to contact us or visit the following offices:

1. Conservation Commissioner
Tanzania Wildlife Management Authority
Dar es Salaam Road-Kingolwira Area
TAFORI Building
P O Box 265
**MOROGORO -Tanzania**
Tel: +255 23-293424
E-mail: **cc@tawa.go.tz**

2. e-Auction of Hunting Blocks Help Desk Tanzania Wildlife Management Authority Phone: +255 784 999 191; +255 717 187 156; +255 754 043 280

**E-mail: e-auctionhuntingblocks@tawa.go.tz**

## TOURIST HUNTING BLOCKS AVAILABLE FOR AUCTIONING

### GROUP A: 26 BLOCKS WHICH THEIR TENURE WILL COMMENCE IMMEDIATELY AFTE THE AUCTIONING EXERCISE

| No. | NAME OF HUNTING BLOCK | SIZE (Sq $Km^2$) | CATEGORY | ECOSYSTEM |
|---|---|---|---|---|
| | CATEGORY I | | | |
| 1 | Kizigo GR (E) 2 | 1287 | I | Ruaha-Rungwa |
| | CATEGORY II | | | |
| 2 | Kizigo GR (E) 1 | 1196 | II | Ruaha-Rungwa |
| 3 | Inyonga GR (C) | 2041 | II | Katavi-Rukwa |
| 4 | Inyonga GR (E) | 3070 | II | Katavi-Rukwa |
| 5 | Kilwa OA S | 852 | II | Selous-Mikumi |
| 6 | Kizigo GR (C) | 1313 | II | Ruaha-Rungwa |
| 7 | Lwafi-Nkamba GR | 3320 | II | Katavi-Rukwa |
| 8 | Moyowosi GR (N 1) | 1392 | II | Malagarasi-Muyovosi |
| 9 | Moyowosi/Njingwe G.R 1 | 1781 | II | Malagarasi-Muyovosi |
| 10 | Muhesi GR | 2633 | II | Ruaha-Rungwa |
| 11 | Piti GR W | 1072 | II | Katavi-Rukwa |
| 12 | Selous GR MT1 | 307 | II | Selous-Mikumi |
| 13 | Ugalla-Msima East | 2099 | II | Malagarasi-Muyovosi |
| 14 | Ugalla-Msima West | 2104 | II | Malagarasi-Muyovosi |
| 15 | Mlele GCA N | 1252 | II | Katavi-Rukwa |
| | CATEGORY III | | | |
| 16 | Chunya OA (E) | 730 | III | Ruaha-Rungwa |
| 17 | Liparamba GR | 617 | III | Selous-Mikumi |
| 18 | Litumbandyosi O.A./Gezamasua | 1346 | III | Selous-Mikumi |
| 19 | Lukwika-Lumesule GR. | 402 | III | Selous-Mikumi |
| 20 | Magwamila O.A. | 1066 | III | Selous-Mikumi |
| 21 | Msanjesi GR | 600 | III | Selous-Mikumi |
| 22 | Muhuwesi G.C.A. | 1438 | III | Selous-Mikumi |
| 23 | Piti OA (E) | 1822 | III | Katavi-Rukwa |
| 24 | Rungwa (N) O.A. | 1515 | III | Ruaha-Rungwa |
| 25 | Wembere South | 5430 | III | Ruaha-Rungwa |
| 26 | Kitwai South West | 1473 | III | Tarangire-Manyara |

### GROUP B: 49 BLOCKS WHICH THEIR TENURE WILL COMMENCE ON 1ST JANUARY 2023

| No. | NAME OF HUNTING BLOCK | SIZE (Sq $Km^2$) | CATEGORY | ECOSYSTEM |
|---|---|---|---|---|
| | CATEGORY I | | | |
| 1 | Burko OA | 712 | I | Lake Natron |
| 2 | Kizigo GR W | 1296 | I | Ruaha-Rungwa |
| 3 | Lake Natron GCA S | 1768 | I | Lake Natron |
| 4 | Lake Rukwa GR | 2040 | I | Katavi-Rukwa |
| 5 | Lolkisale GCA | 739 | I | Tarangire-Manyara |
| 6 | Masai OA W | 877 | I | Tarangire-Manyara |
| 7 | Mto wa Mbu GCA | 1208 | I | Lake Natron |
| 8 | Rungwa Ikili GR | 1084 | I | Ruaha-Rungwa |
| 9 | Rungwa Mpera GR | 2068 | I | Ruaha-Rungwa |
| 10 | Rungwa Rungwa GR E | 1431 | I | Ruaha-Rungwa |
| 11 | Rungwa Rungwa GR W | 1344 | I | Ruaha-Rungwa |
| | CATEGORY II | | | |
| 12 | Chunya Lukwati OA | 2344 | II | Katavi-Rukwa |
| 13 | Chunya Msami OA | 1496 | II | Katavi-Rukwa |
| 14 | Kilombero Ruhuji Ifinga (W) | 2199 | II | Selous-Mikumi |
| 15 | Kilwa OA Mbwemkuru | 1426 | II | Selous-Mikumi |
| 16 | Kilwa OA Nakiu | 1841 | II | Selous-Mikumi |
| 17 | Kitwai GCA SE | 1146 | II | Tarangire-Manyara |
| 18 | Lake Natron GCA N | 1955 | II | Lake Natron |
| 19 | Lake Natron GCA W | 1781 | II | Lake Natron |
| 20 | Longido GCA N | 591 | II | Lake Natron |
| 21 | Luganzo GR | 5217 | II | Malagarasi-Muyovosi |
| 22 | Lukwati GR N | 1757 | II | Katavi-Rukwa |
| 23 | Lukwati GR S | 2058 | II | Katavi-Rukwa |
| 24 | Lunda Nkwambi GCA N | 1046 | II | Ruaha-Rungwa |
| 25 | Masai OA E | 1895 | II | Tarangire-Manyara |
| 26 | Mlele GCA S | 1251 | II | Katavi-Rukwa |
| 27 | Monduli Juu OA | 696 | II | Lake Natron |
| 28 | Moyowosi GR S | 3077 | II | Malagarasi-Muyovosi |
| 29 | Moyowosi/Njingwe G.R 3 | 1782 | II | Malagarasi-Muyovosi |
| 30 | Ngaserai OA | 591 | II | Lake Natron |
| 31 | Rungwa Mwamagembe GR | 997 | II | Ruaha-Rungwa |
| 32 | Rungwa Mzombe OA | 1933 | II | Ruaha-Rungwa |
| 33 | Rungwa OA S | 1679 | II | Ruaha-Rungwa |
| 34 | Ruvu Masai GCA | 2477 | II | Selous-Mikumi |
| 35 | Selous GR LR1 | 1110 | II | Selous-Mikumi |
| 36 | Selous GR LR2 | 1146 | II | Selous-Mikumi |
| 37 | Selous GR LR3 | 1146 | II | Selous-Mikumi |
| 38 | Selous GR MA1 | 1685 | II | Selous-Mikumi |
| 39 | Selous GR MHJ3 | 1147 | II | Selous-Mikumi |
| 40 | Selous GR MS1 | 1343 | II | Selous-Mikumi |
| 41 | Selous GR U3 | 779 | II | Selous-Mikumi |
| 42 | Selous GR U4 | 683 | II | Selous-Mikumi |
| 43 | Ugalla GR E | 1865 | II | Malagarasi-Muyovosi |
| 44 | Ugalla GR S | 1446 | II | Malagarasi-Muyovosi |
| | CATEGORY III | | | |
| 45 | Makere-Uvinza OA | 2565 | III | Malagarasi-Muyovosi |
| 46 | Kilombero Ruhudji/Ifinga (E) | 2310 | III | Selous-Mikumi |
| 47 | Simanjiro GCA W | 1254 | III | Tarangire-Manyara |

**Issued by:**

**Conservation Commissioner**
**Tanzania Wildlife Management Authority - TAWA**
**Morogoro Road-Kingolwira Area**
**TAFORI Building**
**PO Box 2658**
**Morogoro - Tanzania**
**Tel: +255 (0) 23-293424**
**E-mail: cc@tawa.go.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Yanga Princess, Simba Queens mechi 'darasa'

**LIGI** Kuu ya Wanawake Tanzania imeingia katika raundi ya nne na leo mashabiki wa soka wanatarajia kushuhudia mechi itakayowakutanisha watani wa jadi hapa nchini, Yanga Princess dhidi ya wageni, Simba Queens, wote kutoka jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo itakuwa ya kwanza kwa msimu huu wa 2021/22 na inatarajiwa kuchezwa kuanzia saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

Kama ilivyo kaka zao Simba na Yanga wanapokutana, 'joto' kutoka kwa viongozi, wachezaji na mashabiki hupanda, vile vile hali hiyo imeanza kuonekana wakati 'kinadada' hao wanapokutana katika mechi hizo za ligi.

Simba Queens iliyotangulia kupanda daraja, imekuwa na rekodi nzuri dhidi ya watani zao, ikitoa vichapo katika michezo yote miwili katika msimu wa 2019/2020 halafu ikatoka sare na kushinda mchezo wa marudiano msimu uliopita na leo watakutana kwa mara ya tano tangu kuanzishwa kwa ligi hiyo.

Mabingwa watetezi, Simba Queens watashuka dimbani wakiwa kileleni baada ya kushinda mechi zake tatu zilizotangulia, tena kwa idadi nono ya mabao wakati Yanga iko katika nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 12 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

Mbali na kila timu kuhitaji ushindi ili kuendelea kujiimarisha katika vita ya kuwania ubingwa, lakini mechi hii inachukuliwa kama 'kioo' cha soka la wanawake hapa nchini.

Timu zote mbili zimeboresha vikosi vyao, ingawa kila timu imeondokewa na nyota wake waliokuwa katika kikosi cha kwanza msimu uliopita, Simba Queens ikiuza nje ya nchi wakati Yanga Princess ikizidiwa dau na klabu nyingine za hapa hapa Tanzania zilizojipanga kuonyesha ushindani. Mechi ya leo ina mambo mbalimbali ya kujifunza kuanzia kwa wachezaji, makocha pamoja na wadau wote wa soka nchini ambao wamekuwa wakihudhuria michezo mingine ya wanaume.

Kwa sababu mechi hii inatarajiwa kuonyeshwa mubashara na Kituo cha Azam Media, basi wachezaji wahakikishe wanacheza kwa viwango vya juu ili kutumia fursa ya mchezo huo kutangaza vipaji walivyonavyo kama ambavyo wanaume wanavyofanya.

Tunawakumbusha wachezaji wa Simba Queens na Yanga Princess kuibeba heshima ambayo wanaipata ya kuonekana mubashara, ripoti zinasema hakuna nchi nyingine Afrika ambayo mechi za Ligi ya Wanawake zinaonyeshwa mubashara, kwa maana hiyo nafasi ambao wamezipata timu hizi itendewe haki.

Kila mchezaji anatakiwa kufahamu mbali na kuonekana wakiwa na timu za Taifa (Twiga Stars na Tanzanite), mchezo huu ni daraja lingine kwao la kuwashawishi mawakala na makocha kuwatafutia timu katika mataifa mengine ya Afrika au barani Ulaya.


Kama imewezekana kwa Mwanahamisi Omary 'Gaucho' na Enekia Lunyamila kusajiliwa huko Morocco, basi ule mchakato wa mshambuliaji wa Simba Queens, Oppa Clement kuelekea Israel na wengine kuonekana unaweza kutimia endapo watajituma na kuonyesha kandanda safi.

Tunaamini ili ndoto za wachezaji hawa kwenda kucheza soka la kulipwa zitimie, ni lazima waonyeshe nidhamu na si kila mchezaji ataibeba timu yake, lakini atawaachia 'maswali' wafuatiliaji wa mechi hiyo na hatimaye kile kilichowachelewesha kwenda kusakata kandanda ya kulipwa kikamalizika. Nidhamu itakayoonyeshwa si tu itawajenga wachezaji, lakini pia itasaidia kuwavutia wadhamini ambao wanahitajika katika kusaidia maendeleo ya soka la wanawake hapa nchini.

Ni imani yetu makocha waliopewa dhamana ya kuziongoza timu hizo mbili, Edna Lema kwa upande wa Yanga Princess na Sebastian Mkoma anayewaongoza mabingwa watetezi, kuwatendea haki mashabiki wao kwa kupanga vikosi vitakavyoonyesha soka safi kutokana na vipaji walivyonavyo wachezaji wa timu hizo mbili.

Pia tunaamini waamuzi watakaopewa dhamana ya kuichezesha mechi hiyo watatafsiri vyema sheria zote 17 za mchezo huo ili timu itakayostahili kupata ushindi au sare ipate.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba inapowajaribu 'maproo' dirisha dogo

**WAKATI** bado dirisha dogo halijafungwa, hadi kufikia jana jioni, vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga bado haijafanya usajili wa mchezaji yoyote wa kigeni na badala yake imewasajili nyota wanne wa Kitanzania.

Wachezaji hao ni Salum Aboubakar 'Sure Boy' kutoka Azam FC, Dennis Nkane (Biashara United), Aboutwalib Mshery (Mtibwa Sugar) na Crispin Ngushi wa Mbeya Kwanza FC.

Inawezekana kabisa Yanga inajua kwa sasa huwezi kumpata mchezaji yoyote bora kutoka nje ya nchi.

Ingawa inawezekana wapo wachache, lakini ni wale ambao, labda walikuwa majeruhi kwa muda mrefu na sasa wamepona, hivyo hawana timu. Au wale ambao walikuwa na timu lakini wamevunja au wameachwa na klabu zao za zamani kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo mishahara, nidhamu au vitu vingine vinavyofanana na hivyo.

Ni kwamba kwa kipindi hiki wachezaji wazuri wengi wana timu. Mchezaji mzuri na mwenye viwango vya juu, ni lazima awe anachezea timu yoyote inayocheza Ligi ya Mabingwa Afrika au Kombe la Shirikisho Afrika, au timu ambazo tayari zimeshatolewa.

Kifupi wengi wana mikataba na ukitaka umtoe kwenye klabu yake ni lazima uvunje benki. Si pesa ya kitoto. Nadhani pia Yanga kwa sababu haishiriki michuano ya kimataifa msimu huu, basi wala haikuwa na haja hiyo.

Klabu ya Simba ambayo imeingia kwenye hatua makundi ya Kombe la Shirikisho, yenyewe ina mahitaji ya wachezaji. Ni lazima iongeze wachezaji ambao wanaona wanaweza wakawasaidia kwenye michuano hiyo.

Kwa kujua kabisa kuwa hiki ni kipindi cha dirisha dogo la usajili na mara nyingi kunakuwa na hakuna wachezaji wengi wazuri, sidhani kama hawako sahihi kuwajaribisha.

Mimi nadhani kipindi cha dirisha kubwa kwa sababu kunakuwa na wachezaji wazuri ambao mikataba yao imekwisha na kuna biashara kubwa ya usajili, klabu inaweza kusajili wachezaji bila kuwajaribisha. Kwa sababu itasajili wachezaji inaowafahamu na imewaona wakicheza katika klabu zao.

Kipindi hiki ambacho Simba inahitaji wachezaji, ina haki ya kuwajaribisha kabla ya kuwasajili ili isije kuingia mkenge, kwani tumeona huko nyuma klabu mbalimbali zikiwamo Simba, Yanga na Azam zilivyofanya usajili kama huo wa dirisha dogo ukawagharimu.

Kuna baadhi ya wachambuzi wa michezo wamekuwa wakibeza juu ya klabu hiyo kuwaleta wachezaji kwa ajili ya majaribio. Wanadai klabu kubwa kama Simba inatakiwa isajili wachezaji ambao tayari wapo tayari kucheza moja kwa moja.

Kama nilivyosema, ni kipindi kigumu sana kupata wachezaji hao. Kama ingekuwa dirisha kubwa ningeungana nao. Hata kama ni mchezaji kama Sharaff Eldin Shiboub ambaye ameshawahi kuichezea Simba lakini ni lazima Kocha Mkuu, Pablo Franco ajidhihirishe kama anafaa au vipi. Inawezekana akawa yupo kwenye kiwango kile kile kama ilivyokuwa huko nyuma, lakini kocha bado akasema hamhitaji.

Kutokana na mashindano ambayo timu hiyo inakwenda kucheza, huenda Simba inaona inahitaji wachezaji wa nje na si wa ndani, ndiyo maana mpaka sasa haijasajili mchezaji yoyote mzawa, ingawa muda bado.

Kwa maana hiyo naona tu tuwaache Simba wafanye wanavyoona badala ya kuanza kuwabeza, kwani sidhani kuna kosa kubwa ambalo wanafanya.

Kitu ambacho hawataki ni kupoteza pesa kwa kusajili mchezaji ambaye hana kiwango au alikuwa na kiwango zamani, lakini kwa sasa hayupo vizuri.

Tuliona huko nyuma kuwa wachezaji kama Yikpe Gnamien wa Yanga ambaye Kocha Mkuu wa Yanga wakati huo, Charles Mkwasa alipotaka afanyiwe majaribio, lakini yeye na wakala wake alikataa, kitu ambacho kiliwafanya viongozi wa timu hiyo kumpa mkataba haraka bila matakwa ya mwalimu, wote wanajua kilichotokea.

Na kumfanyia majaribio mchezaji si kama hajui, ila ni kujidhihirisha uwezo wake wa wakati husika, kwani mara nyingi viongozi na makocha huletewa video fupi zilizohaririwa vizuri au sifa za miaka mitano nyuma, lakini ukweli ni kwamba kwa wakati huo uwezo umeshuka kwa sababu mbalimbali, ikiwemo umri au majeraha.

Cha ajabu ninachoona ni wachezaji wetu nchini wakienda kwenye klabu za nje kwa majaribio, baadhi ya wachambuzi hao hao hufurahi na kusema soka letu linakua, lakini klabu zetu zikipokea wachezaji kutoka nje ya nchi kuja kufanya marajibio wanaponda.

# Ardhi yazindua kituo mawasiliano wateja

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WIZARA ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imezindua kituo cha Mawasiliano kwa Wateja kwa lengo la kuondoa kero za wananchi katika masuala ya ardhi.

Uzinduzi huo ulifanywa jana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, katika ofisi za wizara zilizoko Mtumba jijini Dodoma.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Waziri Lukuvi alisema kwa kutumia maendeleo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), wizara yake imeona kuna baadhi ya huduma za ardhi zinazoweza kutolewa kwa njia ya simu na mitandao ya kijamii ambazo hazimlazimu mwananchi kufika ofisi za ardhi.

''Wizara imeanzisha kituo cha mawasiliano kwa wateja kitakachotoa huduma ya mawasiliano moja kwa moja na mwananchi kwa kutumia simu na ujumbe wa maneno kupitia WhatsApp ambapo majibu au ufafanuzi utatolewa kwa wananchi na wataalamu wa ardhi," alisema.

Kwa mujibu wa Lukuvi, kituo hicho kina wataalamu wabobezi katika masuala ya ardhi waliopata mafunzo yakinifu ya kuifanya kazi ya kutoa huduma kwa wateja kwa weledi na kutoa majibu kwa wakati.

Pia alitumia fursa ya uzinduzi wa kituo hicho kuwataka wananchi kukitumia kuwasilisha kero mbalimbali zikiwamo za matapeli wa ardhi, watumishi wa sekta ya ardhi wasio waaminifu pamoja na wale madalali wanaochukua fedha za wapangaji na kusisitiza kuwa anayepaswa kutoa fedha kwa madalali ni mwenye nyumba na si mpangaji.

Alisema kupitia kituo hicho mwananchi atalazimika kupiga simu na kuongea moja kwa moja na watoa huduma kupitia namba 0739-646-885 au kutuma ujumbe wa maneno kupitia mtandao wa WhatsApp kwa namba hizo. Kituo hicho kitakuwa wazi siku za kazi kuanzia saa 2:00 asubuhi hadi saa 9:00 alasiri kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi.

''Ni matumaini yangu kituo hiki kitatoa fursa kwa wananchi kupata huduma za ardhi kwa haraka, kwa ufanisi na kwa gharama nafuu kwa kuwa mwananchi hatakazimika kufika ofisi za ardhi endapo huduma anayohitaji anaweza kuipata kupitia simu," alisema.

Uanzishwaji Kituo cha Mawasiliano kwa Wateja ni moja ya mikakati mbalimbali ya wizara kuhakikisha huduma kwa wateja wa ardhi zinaboreshwa na zinatolewa kwa weledi na ufanisi mkubwa.

# Mbunge atamba kumaliza tatizo la maji

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, amesema tatizo la maji katika baadhi ya maeneo ya Manispaa ya Morogoro, litakwisha baada ya muda mfupi kutokana na kukamilika kwa miradi mikubwa minne.

Miradi hiyo mikubwa ambayo fedha zake zimetolewa na serikali kuu ni pamoja na Bigwa – Bohomela, Bigwa – Kilakala, Mamboga – Mkundi na Kasanga ambapo fedha zake zimetokana mpango wa fedha za UVIKO- 19.

Abood alitoa ahadi hiyo kwa wananchi jana baada ya kukagua na kuridhishwa hatua iliyofikiwa inayotekelezwa katika maeneo tofauti na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MOROWASA).

Akizungumza baada ya kukagua miradi hiyo, Abood alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha za miradi ya maji kwa Manispaa ya Morogoro ambazo zitawezesha kumaliza tatizo la maji hasa katika maeneo ya pembezoni mwa mji.

"Wakazi wa Manispaa ya Morogoro wategemee mafanikio mazuri ya kupunguza kero ya maji baada ya muda mfupi kukamilika kwa miradi mikubwa ya maji tuliyopewa fedha na Rais Samia," alisema.

Alitaja baadhi ya miradi iliyopatiwa fedha ni Bigwa – Bohomela utakaogharimu Sh. bilioni 2.4 unaotarajia kukamilika Januari 15, mwaka huu na mradi wa Mambogo ambao ni wa usambazaji wa mabomba ya maji hadi kwenye tangi lenye ujazo wa lita milioni mbili lililojengwa eneo la Mkundi kwa gharama ya Sh. bilioni 1.4 ambalo litahudumia zaidi ya wakazi 130,000 wa kata za Mkundi na Lukobe.

Mbunge huyo alitaja mradi mwingine utakaomaliza kero ya maji ni wa Bigwa – Kilakala na unaofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) ikiwa ni mkopo wa euro milioni 70 ambao utapanua uwezo wa Bwawa la Mindu kuongeza kiwango cha maji.

Hata hivyo, mbunge huyo aliwataka wananchi kuacha tabia ya kuharibu vyanzo vya maji na pia kushiriki kupanda miti katika maeneo mbalimbali ili vyanzo vya maji viendelee kuwepo.

"Tunapoharibu vyanzo vya maji, hatuna wa kumlaumu tena. Niwaombe wakazi wa Manispaa ya Morogoro tupande miti kwa wingi na kuvitunza vyanzo vya maji ili tuwe na uhakikika wa kupata maji," alisema Abood.

Kaimu Meneja wa Ufundi wa MOROWASA, Mhandisi Victor Ngowi, alisema kwa sasa wanatekeleza miradi ya muda mfupi yenye thamani ya Sh. bilioni 10 ambayo itakapokalimika itatatua tatizo la upatikanaji wa maji katika makazi mapya zikiwamo kata za Mkundi na Lukobe.

Mhandisi Ngowi pia alisema MORUWASA imepewa miradi miwili ya maji kupitia fedha za UVIKO-19 ukiwamo wa Kasanga wenye thamani ya Sh. milioni 616 na mkandarasi tayari anaendelea na kazi kwa ajili ya kumaliza kero hiyo ya maji.



Mbunge wa Morogoro Mjini, AbdulAziz Abood mbele akishuka kutoka katika tangi la maji lenye ujazo wa lita milioni 2 lilojengwa eneo la Mkundi na Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira (MOROWASA), kwa ajili ya kusambaza maji katika eneo la Mkundi na Lukobe, baada ya kukagua mradi huo jana. Wengine ni Watalaamu wa mamlaka hiyo. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# TIC yatoa vyeti motisha kwa wawekezaji wazawa na wageni

**Na Joseph Mwendapole**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimeanza kutoa hati za motisha kwa wawekezaji mbalimbali kama sehemu ya mkakati wa kuhamasisha uwekezaji hapa nchini.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na TIC, hati hizo zinatolewa kwa mujibu wa mamlaka iliyopewa na Sehemu ya Tatu ya Sheria ya Uwekezaji Kifungu cha 17 (1-8). "Haya yanafanyika kwa mujibu wa sheria na wenye cheti cha motisha wanastahili kupata vivutio mbalimbali vya uwekezaji kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 na tunafanya hivi kuvutia wawekezaji zaidi," ilisema taarifa hiyo.

Kampuni zinazojihusisha au zinazokusudia kujihusisha na sekta za madini na petroli zitafuata utaratibu wa uidhinishaji ulio katika sheria zao yaani Sheria ya Madini ya 2010 na Sheria ya Petroli ya 2015.

"Hata hivyo, kituo kinapoombwa kitawasaidia wawekezaji wote kupata vibali na idhini inayotakiwa na sheria nyingine kuanzisha na kuendesha uwekezaji nchini Tanzania," ilisema taarifa hiyo.

Pia taarifa ilisema kwa wawekezaji wa ndani, kiwango cha chini cha thamani ya uwekezaji kwa miradi kinapaswa kuwa angalau dola za Marekani 100,000 kwa miradi ambayo inamilikiwa kikamilifu na raia wa Tanzania.

Ilisema kwa wawekezaji wa kigeni thamani ya chini ya uwekezaji wa mradi inapaswa kuwa angalau Dola za Marekani 500,000 kwa miradi ambayo inamilikiwa kabisa na wawekezaji wa kigeni au ikiwa ni ubia.

Aidha, taarifa ilisema ili mwekezaji apate hati ya motisha, lazima awe na nakala iliyoidhinishwa ya cheti cha usajili wa kampuni, nakala ya mkataba/Katiba ya kampuni na nakala za Muungano, fomu za maombi za TIC zilizojazwa kikamilifu ambazo hutolewa na kituo.

Pia ilisema lazima mwekezaji aonyshe mpango wa biashara wa mradi/andiko la mradi wa uwekezaji, ushahidi wa mtaji wa kutosha wa fedha ili kutekeleza mradi, ushahidi wa eneo la mradi, azimio la bodi ya kampuni kusajili mradi na TIC na barua ya maombi ambayo itaambatanishwa na nyaraka tajwa hapo juu.

Ilisema kitengo cha huduma ya Aftercare ni kitengo cha msingi cha utendaji kazi katika kukuza, kuvutia na kuwezesha uwekezaji, ambacho jukumu lake la kuwezesha uanzishaji na kusababisha uendelevu wa uwekezaji kwa nia ya kuongeza mchango wake katika maendeleo ya uchumi Nchini.

"Kitengo cha huduma kwa wawekezaji hutoa huduma kadhaa za kuwezesha mradi uliosajiliwa wa uwekezaji baada ya kusajili mradi wako, kitengo hiki kinatoa usaidizi katika kuhakikisha kuwa mradi wako wa biashara unatekelezwa bila vizuizi visivyo vya lazima. Ikumbukwe kuwa tangu kuanzishwa kwake (TIC) imekuwa na mafanikio makubwa katika kuwezesha kuanza kwa uwekezaji," alisema.

# Ujenzi wa daraja wamfurahisha DC

**Na Steven William,** IRINGA

UJENZI wa daraja kubwa linalounganisha kata tatu wilayani Iringa, umefikia asilimia 70, hivyo wananchi kuipongeza serikali kwa utekelezaji wa mradi huo.

Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo, juzi alitembelea na kukagua mradi huo katika kata ya Ifunda na kupata taarifa ya mradi.

Alisema daraja hilo linaunganisha kata za Ifunda, kata ya Madhana na Kihanga na kwamba ujenzi wa daraja hilo umefikia asilimia 70 kukamilika ujenzi wake.

Moyo alisema ujenzi wa daraja hilo kubwa unatekelezwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) wilayani Iringa na kupongeza kwa kiwango ujenzi ulipofikia.

Mkuu wa wilaya alisema kukamilika kwa ujenzi wa daraja hilo, kutasaidia sana wananchi wanaoishi katika kata hizo kutumia miundombinu hiyo na barabara kutoa mazao yao vijijini kupeleka sokoni Iringa mjini.

Katika hatua nyingine, Moyo aliwaambia wananchi kwamba wilaya ya Iringa iko mbioni kukamilisha ujenzi wa madarasa katika shule za sekondari 66 zikiwamo shule shikizi 28 ili wanafunzi wanaoanza kidato cha kwanza mwakani waingie katika madarasa.

Alisema kuwa katika wilaya ya Iringa, wanajenga vyumba vya madarasa 66 katika shule za sekondari na shule shikizi 28 na kwamba baadhi ya shule ujenzi wa madarasa umefikia hatua za mwisho kwa kuweka madirisha ya vioo.

Moyo alisema wakati wowote kuanzia sasamafundi watakabidhi vyumba hivyo vya madarasa kwa kuwa ujenzi umefikia hatua za mwisho baadhi ya sekondari na zile shule shikizi.



Meneja Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA) Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Julietу Payovela (katikati), akisaini mikataba ya utekelezaji wa miradi 10 ya maji yenye thamani ya Sh. bilioni 4.3 inayotekelezwa kwa fedha za UVIKO-19, mkoani humo, jana. Kulia ni mmoja wa wakandarasi watakaotekeleza miradi hiyo, John Ntalimbo kutoka Kampuni ya Jonta na (kushoto) ni Meneja wa RUWASA wilaya ya Kishapu, Dicskon Kamanzima. **PICHA: MARCO MADUHU**

# RC awapa kibarua watendaji wanafunzi kuripoti shuleni

**Na Julieth Mkireri,** MKURANGA

MKUU wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, amewataka watendaji walioko mkoani humo kuhakikisha watoto wote wanaostahili kuanza shule Januari 17, mwaka huu, wanaripoti katika shule walizopangiwa.

Kunenge alisema hayo juzi alipokuwa akikagua maendeleo ya miradi ya sekta ya elimu katika wilaya ya Mkuranga ambayo inatekelezwa kwa fedha za maendeleo ya miradi kwa ustawi wa taifa zilizotolewa na serikali.

Pia alipiga marufuku wazazi wenye tabia ya kuwapeleka watoto wao kuchunga ng'ombe na kuwataka kuacha vitendo hivyo kwa kuwa serikali imejenga miundombinu mizuri ili watoto wa kitanzania wapate haki ya kusoma. Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amefanya kazi ya kutafuta fedha na hatimaye kupata mkopo usio na riba kwa lengo la kujenga miundombinu ya elimu na afya, hivyo hategemei kuona kuna watoto wanaotakiwa kuwa shuleni wako mitaani.

Kunenge alisema mkoa wa Pwani umenufaika kwa kupata Sh. bilioni 13.39 na kati ya hizo Sh. bilioni 10.9 zimetumika kwa ujenzi wa vyumba vya madarasa ya kidato cha kwanza na madarasa Shikizi.

Alisema mkoa huo umejenga madarasa 535 yakiwamo madarasa ya sekondari kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha kwanza 422 na madarasa shikizi 133 na kwamba vyumba vya madarasa sita ya shule shikizi yanatarajiwa kukamilika hivi karibuni.

Kwa mujibu wa Kunenge, wanafunzi 32,399 wataanza masomo Januari 17, mwaka huu, kwa hiyo lazima watoto wote waripoti ili Rais apate moyo wa kuendelea kutafuta fedha zingine kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kwa faida ya nchi na wananchi wake.

"Nampongeza Rais kwa kutafuta fedha hizi za mkopo usio na riba na namwomba akipata mkopo mwingine azidi kuuangalia mkoa wa Pwani lakini sote tunajua fedha hizi zimewekwa wazi na hapakuwa na usiri wowote. Kwa hiyo niwaombe madiwani na watendaji toeni elimu kwa wananchi juu ya matumizi ya fedha hizo," alisema.

Katika ziara hiyo, Kunenge alikagua Shule ya Msingi Jamhuri iliyoko kata ya Vikindu iliyojengwa madarasa sita pamoja na Shule ya Sekondari Dundani kayika kata ya Mkuranga.

Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Ally, alisema kuna kila sababu ya kumpongeza Rais kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kuwa amekuwa mkombozi wa wananchi wa wilaya ya Mkuranga na kwamba lazima wananchi wafahamu juhudi hizo.

Alisema wilaya ya Mkuranga ndiyo pekee katika mkoa wa Pwani iliyofaidika kwa kujenga madarasa mengi. Imejenga madarasa 151 yatakayotumika na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

# Washindi 100 NMB Wanyakua mamilioni

**Na Mwandishi Wetu**

Wateja 100 wa kwanza wa kampeni ya NMB MastaBata-Kivyako Vyako walipatikana jana na kuzawadiwa pesa taslimu TZS 100,000 kila mmoja na taasisi hiyo kiongozi wa shughuli za kifedha nchini.

Washindi hao wamezawadiwa jumla ya Sh. milioni 10 katika promosheni hiyo iliyozinduliwa rasmi katikati ya Desemba, mwaka jana, kwa lengo la kuchagiza matumizi ya kadi za malipo za Mastercard kama sehemu ya mchango wa NMB katika juhudi za taifa za kujenga uchumi usio tegemea sana fedha taslimu.

NMB pia inatumia kampeni hii kuendeleza uchumi wa kidijitali kurudisha fadhila kwa wateja wake waaminifu ambao wamekuwa mhimili muhimu wa safari yake ya mabadiliko ya kidijitali.

Akizungumza wakati wa droo ya kuwapata washindi wa kwanza wa MastaBata-Kivyako Vyako, Meneja Mwandamizi wa Wateja Binafsi wa NMB, Ali Ngingite, alisema zaidi ya Sh. milioni 200 zitanyakuliwa kwenye kampeni hii ya miezi mitatu.

"Hili ni toleo la tatu la kampeni za MastaBata zilizoanza rasmi mwaka 2018 kuwahamasisha wateja na wasio wateja wa NMB kutumia kadi za Mastercard wanapofanya malipo na miamala kupitia intaneti," alisema.

"Kama watangulizi wake, promosheni ya MastaBata-Kivyako Vyako pia ina lengo la kuwatambua na kuwazawadia wateja wetu waaminifu kwa kuendelea kutumia huduma zetu," aliongeza Ngingite na kutanabaisha kuwa zitakuwapo pia droo za kila mwezi na ile kubwa ya mwisho.

Wakati washindi 100 wa kila wiki watashinda Sh. 100,000 kila mmoja, 25 watanyakua Sh. 1,000,000 kila mwezi na 30 wa mwisho watashinda jumla ya Sh. milioni 90, zikiwa ni Sh. milioni kwa kila mshindi.

Ngingite alisema takribani wateja 1,000 wanategemewa kushinda zawadi za promosheni ya Masta-Bata-Kivyako Vyako iliyopangwa kufikia tamati Machi, mwaka huu.

Kampeni hii inawahusisha pia wateja wa benki hiyo wanaofanya malipo kwa NMB MasterPass QR.

Kama kawaida droo ya jana ilisimamiwa na Ofisa mwandamizi wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT). NMB inasema kampeni zake za MastaBata zimefanikiwa sana.



## Askofu amshauri Rais Samia kutosikiliza maneno ya wanasiasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Maombi na Maombezi kwa Mataifa yote (Reaching Unreached Tanzania) RUTACH, Living Mwambapa, amemshauri Rais Samia Suluhu Hasan kutosikiliza maneno ya kukatisha tamaa ya wanasiasa uchwara.

Askofu Mwambapa, alibainisha hayo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma.

Alisema Rais Samia anatakiwa kuwapuuza baadhi ya watendaji ndani ya serikali na kuendelea kufanya kazi kama ilivyo kaulimbiu yake ya Kazi Iendelee.

"Wanaobeza utendaji wa Rais Samia wanatafuta kiki za kisiasa mwaka 2025 lakini wanashindwa kutambua kuwa hakuna serikali yoyote duniani isiyokopa kwa ajili ya maendeleo.

"Ukikopa kwa ajili ya maendeleo hapo shida iko wapi Watanzania wanahitaji kuona maendeleo na inapotokea mtu anabeza anakuwa na tatizo binafsi,"alisema Askofu Mwambapa. Alisema ushauri wake kwa Rais Samia ni kwamba atasikia mambo mengi na kuona mambo mengi katika kuelekea uchaguzi mkuu mwaka 2025, lakini anatakiwa kuendeleza juhudi zake za kutafuta maendeleo ya wananchi anaowaongoza.

Kauli ya Askofu Mwambapa inakuja baada ya aliyekuwa Spika wa Bunge Job Ndugai kutangaza kujiuzulu nafasi yake.

Sehemu ya kauli ya Ndugai iliyoibua gumzo katika mitandao ya kijamii ni pamoja na kuwataka Watanzania wapime iwapo mwaka 2025 watapenda kuendelea na uongozi unaopenda kukopa au kuenda na wale ambao wanapenda kufanya maendeleo kwa kutumia vyanzo vya ndani.

# Magonjwa yasiyoambukiza bado ni tatizo nchini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

RIPOTI ya mwaka 2020 ya Takwimu za Kamisheni ya Umasikini na Magonjwa imeonyesha kuwa asilimia 41 ya utafiti uliofanyika nchini katika kipindi hicho ni kuhusu magonjwa yasiyoambukiza na majeruhi.

Pia imeonyesha Tanzania imekuwa ikitumia Dola za Marekani milioni 700 kugharamia katika kukinga na kutibu magonjwa hayo kwa mwaka.

Akizungumza katika mkutano wa kutoa ripoti ya matokeo ya utafiti katika sekta ya afya uliofanywa na watafiti mbalimbali hapa nchini, Prof. Goodluck Makundi, alisema magonjwa yasiyo ya kuambukiza hapa nchini bado ni changamoto.

"Kuna ongezeko la magonjwa yasiyoambukizwa hapa nchini na kufikia vifo, ongezeko hili ni mara mbili ya hali ilivyokuwapo mwaka 2015 hali hii inasababisha nguvu kuelekezwa zaidi katika kutibu kuliko kukinga na ni ghali kutibu kuliko kukinga."alisema.

Prof. Makundi alisema tatizo hilo haliwapati watu wazima na wazee tu bali hata vijana na watoto wanakumbwa, huku akisema linachangiwa na mabadiliko ya mtindo wa maisha na lishe.

Kadhalika, alisema hilo ni tatizo mtambuka linahusisha sekta mbalimbali.

"Ni changamoto kubwa hapa nchini kwa magonjwa haya yasiyo ya kuambukiza, magonjwa haya ni pamoja na moyo, shinikizo la damu, saratani pamoja na magonjwa ya mfumo wa hewa"alisema.

Prof. Goodluck alitaja baadhi ya vitu vinavyosababisha magonjwa yasiyo ya kuambukiza kuwa ni pamoja na matumizi ya tumbaku, kutofanya mazoezi, ulaji vyakula usiozingatia lishe bora na matumizi ya pombe kupita kiasi.

Alisema Shirika la Afya Duniani (WHO) linasema mambo hayo yanachangia kwa asilimia 80 ya tatizo hilo duniani.

Akizungumzia kuhusu matokeo ya utafiti uliofanywa na watafiti katika sekta ya afya alisema matatizo ya magonjwa hayo yasiyo ya kuambukizwa na majeruhi yanachangia kwa asilimia 41 ya vifo na walemavu.

Vile vile alisema matokeo ya utafiti wao yanaonyesha kuwa pamoja na mambo mengine kuna upungufu wa fedha za kugharamia magonjwa hayo na kwamba asilimia 7.8 ya matumizi ya sekta hiyo ndiyo hutumika ikilinganishwa na tatizo la asilimia 41.

Akitoa mapendekezo katika sekta ya afya alisema inahitaji uratibu wa hali ya juu kwa kutumia ofisi mbalimbali ikiwamo Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), lakini pia sheria na kanuni zilizopo dhidi ya mapambano ya magonjwa yasiyo ya kuambukizwa ziimarishwe.

Vile vile, alisema pendekezo lingine ni kuanza kuzungumzia elimu ya magonjwa haya katika ngazi tofauti tofauti pia yaingizwe kwenye mpango wa elimu ya afya mashuleni.

Katika hatua nyingine alisema viongozi wa dini pia wanao wajibu wa kuelezea angalau kwa dakika chache wawapo katika ibada zao huku akisema hii itasaidia waumini kupata uelewa juu ya magonjwa haya katika maeneo tofauti tofauti na kuwapa uelewa wa kutosha.

Awali akifungua hafla hiyo iliyoandaliwa na Tume ya Sayansi, Teknlojia na Ubunifu (COASTECH) mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa COASTECH, Dk. Wilbert Manyilizu, alisema lengo la warsha hiyo ni kuwashirikisha wadau wakuu wa matokeo ya tafiti za kisayansi na teknolojia ili waweze kuwasilisha na kutoa matokeo ya tafiti zao.

Alisema, COASTECH iliwaita watafiti katika sekta nne za awali ambazo ni sekta ya afya, kilimo, maliasili na mifugo ili wawasilishe utafiti wao ambao hufanyiwa kazi na tume hiyo ambayo ndiyo yenye dhamana ya kuishauri Serikali katika masuala ya sayansi na teknolojia.



Waratibu wa Mradi wa kudahili watoto wenye ualbino na wasioona wa Haki Yangu (MY RIGHT SRF), Emmanuel Mhehwa (kushoto) na Kombo Kombo (kulia), wakiwa wamekaa na watoto wanaofadhiliwa na mradi huo, walipowatembelea kijijini kwao Nhome, wilaya ya Bahi, mkoani Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jenista awataka watumishi kupata chanjo Uviko-19

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama amewataka watumishi wa ofisi hiyo kujitokeza kwa wingi kupata chanjo ya Uviko-19, ili kujilinda na maambukizi ya wimbi la nne.

Alitoa ushauri huo jijini hapa wakati akizungumza na watumishi wa wizara hiyo katika kikao kazi.

Mhagama alisema kuwa dunia inaendelea kupambana na wimbi la nne la Uviko-19 hivyo ni muhimu watumishi wakajikinga na janga hilo kwa kupata chanjo sambamba na kuhamasisha jamii.

Waziri Mhagama alisema watumishi wanatakiwa kuwa mstari wa mbele katika kupata chanjo ikiwa ni pamoja na kuhamasisha jamii kuchanja.

"Watumishi wote mnajua kuwa dunia kwa sasa inahangaika kupambana na Uviko-19 na Tanzania ni miongoni mwa nchi inayopambana kuthibiti gonjwa hilo.

"Ili kuendelea kupambana na kirusi hiki nawaomba watumishi wote muone umuhimu wa kupata chanjo ili kuweza kulinda afya zenu na kulinda afya za watu mnaoishi nao"alisema.

Alisema pamoja na kuwa chanjo ni hiari lakini aliwashauri kila mtumishi apate chanjo kwani atakuwa amejiweka katika nafasi nzuri ya kiafya sambamba na kujikinga na maambukizi mengine mapya.

Aidha, aliwataka watumishi kutoyasikiliza maneno ya kukatisha tamaa juu ya matumizi ya chanjo kwani iko salama kwa matumizi ya binadamu.

"Yapo maneno ya watu ambao wamekuwa wakidai kuwa chanjo ina madhara jambo ambalo siyo kweli kwani tayari wataalamu wa afya wanaweka wazi kuwa chanjo ni salama kwa mtu yoyote hata akiwa mjamzito.

"Aidha mnatakiwa kuzingatia masharti yote yanayotolewa na wataalamu ikiwa ni pamoja na kuvaa barakoa, kunawa mikono kwa maji tiririka,kutumia vitakasa mikono pamoja na kujiepusha na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima"alisisitiza





# KMKM yaanza kukwepa utegemezi serikalini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KIKOSI Maalumu cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimezindua kiwanda kidogo cha kutengeneza mikate ya boflo ambayo ni maarufu visiwani Zanzibar pamoja na ofisi ya malipo ya kielektroniki katika hospitali ya kikosi hicho, Kibweni.

Akizungumza jana katika uzinduzi wa miradi hiyo Makao Makuu ya KMKM, Kibweni, Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema ameridhika na ubora wa majengo pamoja na vifaa. Pia wataalamu watakaotengeneza mikate hiyo ni wapiganaji wa kikosi hicho.

Waziri alisema hatua ya KMKM kukusanya fedha kwa njia ya kielektroniki katika kuhakikisha mapato na makusanyo ya fedha yanadhibitiwa ipasavyo, anatumaini kuwa uchumi wa kikosi hicho utaongezeka.

"Nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa kuiunga mkono serikali ya Zanzibar katika kuinua uchumi na kudhibiti upotevu wa fedha za serikali," alisema.

Tabia alisema mradi wa mikate ambao unazalisha mikate utaongeza kipato kwa kikosi hicho na kupunguza utegemezi kwa serikali, hivyo kuviwezesha vikosi vingine na wananchi kununua mikate katika kikosi hicho.

Alisema juhudi kubwa zilizofanywa na KMKM za kuwekeza katika uzalishaji na kuanzisha miradi, zinapaswa kupongezwa na kuwa mfano wa kuigwa na kuzitaka taasisi zingine kutumia rasilimali zilizopo katika kuwekeza na kupata mapato ili kujiendesha katika shughuli za kila siku.

Wakati serikali inaadhimisha miaka 58 ya Mapinduzi, alisema makusanyo ya fedha kwa njia ya kielektroniki katika Hospitali ya KMKM yatasiadia kwa kiwango kikubwa kukua na kuimarika kwa huduma za afya na tiba katika hospitali hiyo.

"Nawashauri kwamba makusanyo na mapato ya fedha ya hospitali yalenge zaidi katika kuimarisha na kuboresha huduma za hospitali zikiwamo dawa, vifaa tiba, mashine za kisasa, majengo, mafunzo kwa wataalamu wa afya na kuajiri kwa mikataba wataalamu bingwa wa afya katika maeneo ya magonjwa ya figo, moyo, miyonzi, upasuaji wa kifua na moyo, mfumo wa uti wa mgongo, ubongo na ufanisi wa mwili," alisema Tabia.

Alisema serikali inaimani kubwa na hospitali hiyo kwa maana hiyo juhudi za ziada zinahitajika katika kuhakikisha hospitali hiyo inapanda hadhi zaidi na kuwa hospitali ya mkoa.

Naibu Mkuu wa KMKM, Kapteni Khatib Khamis Mwadini, alisema miradi hiyo ni utekelezaji wa malengo ya Mapinduzi ili kudhibiti upotevu wa fedha katika kikosi hicho na kupunguza utegemezi kutoka serikalini.

Alisema maofisa wa kikao hicho wana jukumu la kuhakikisha majengo na vifaa, vilivyopo vinaenziwa, kutunzwa na kutumika vizuri ili kuifanya huduma ya malipo ya fedha kwa njia ya kielektroniki na huduma ya uzalishaji wa mikate kuwa endelevu.



Waziri wa Habari, Vijana, Sanaa, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita akiangalia mikate aina ya boflo, baada ya kuzindua kiwanda cha utengenezaji wa mikate kinachomilikiwa na Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM), jijini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mbarawa asema umeme ajenda ya Mapinduzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, amesema Serikali ya Zanzibar imeyafikia malengo ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964 kwa kufikisha huduma muhimu za kijamii na maendeleo ikiwamo nishati ya umeme na kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi.

Aliyasema hayo juzi wakati akifungua mradi wa nishati ya umeme huko Mkia wa Ngombe, Micheweni mkoa wa Kaskazini Pemba ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Prof. Mbarawa alisema mahitaji ya nishati ya umeme ni makubwa kwa ajili ya kuleta mageuzi ya viwanda na uwekezaji wa miradi katika kisiwa cha Pemba.

Alisema usambazaji umeme katika kijiji cha Mkia wa Ngombe ni mageuzi makubwa ambayo yamelenga kuleta mabadiliko ya wananchi katika sekta mbalimbali zikiwamo uchumi na maendeleo ya uwekezaji. Hatua hiyo, alisema ni sehemu ya utekelezaji wa malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo yalilenga kuwawezesha wananchi kuishi katika maisha bora yanayokwenda sambamba na mageuzi ya kiuchumi na maendeleo.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea kutekeleza malengo ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964 ambayo ahadi zake kubwa ni kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kuona wananchi wake wanaishi maisha bora," alisema.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini ya Serikali ya Zanzibar, Miraji Mgereza Mzee, alisema mradi wa usambazaji wa umeme katika kijiji cha Mkia wa Ngombe unakwenda sambamba na mikakati ya serikali kuona vijiji vyote vinapata nishati hiyo.

Alisema Zanzibar imeshusha bei ya kuunganisha umeme majumbani kwa lengo la kuwawezesha wananchi kupata huduma hiyo na kuleta mabadiliko ya kiuchumi vijijini.

"Tumeshusha viwango vya kuunganisha nishati ya umeme kutoka Sh.400,000 hadi Sh. 200,000 hatua ambayo imewawezesha wananchi kupata huduma hii katika maeneo mbalimbali yakiwamo vijijini," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba, Salama Mbarouk Khatib, alisema wamejipanga kuhakikisha wananchi wanaingiza umeme majumbani kwa ajili ya matumizi sahihi.

Alisema katika mkoa wa Kaskazini Pemba wamefurahishwa na juhudi zilizochukuliwa na serikali za usambazaji wa umeme katika wilaya ya Micheweni ambao utasaidia juhudi za uwekezaji wa miradi mbalimbali katika maeneo huru ya uchumi.

# Dk. Mwinyi ajivunia maendeleo ya elimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema mahitaji ya utoaji elimu yameongezeka ikilinganishwa na miaka 58 iliyopita tangu kufanyika kwa Mapinduzi.

Kutokana na hali hiyo, amesema serikali itatafuta ufumbuzi katika kutatua changamoto za sekta hiyo ikiwamo ujenzi wa vyamba vya madarasa kadri uchumi utakavyoruhusu.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana baada ya kufungua madarasa sita katika Shule ya Msingi Sebleni Wilaya ya Mjini Unguja. Shule hiyo alichangia katika ujenzi wake alipokuwa mbunge wa Kwahani.

Alisema hatua ya ujenzi wa madarasa hayo itapunguza msongamano wa wanafuinzi madarasani na kuwapa mazingira bora ya kujifunza.

"Mahitaji katika utoaji wa elimu ni lazima yataongezeka na changamoto zilizopo zikiwamo za miundombinu, uhaba wa walimu, uhaba wa vitabu, ukosefu wa madawati na mambo mengine ni wajibu wa serikali kuyakabili na kuyapatia ufumbuzi kadri hali ya uchumi itakavyoruhusu," alisema.

Kuhusu historia ya elimu, alisema kabla ya Mapinduzi mwaka 1964, Zanzibar ilikuwa na shule 69 katika ngazi zote za elimu Unguja na Pemba na kati ya hizo, mbili zilikuwa za maandalizi, 62 msingi na tano za sekondari.

Alisema hadi Desemba, mwaka jana, shule zimeongezeka ambapo kwa ngazi ya elimu ya maandalizi ziko 774, msingi 545 na sekondari 302.

Pia alisema katika kuhakikisha hakuna mtoto anekosa fursa ya elimu serikali kwa kushirikiana na Shirika la Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF) na Taasisi ya Education Above All ya Qatar, imetia saini mkataba wa mradi unaogharimu dola za Marekani milioni tatu wenye lengo la kuwarejesha shuleni watoto wenye umri kati ya miaka saba na 14 walio nje ya elimu ama kwa kutoroka au  kutoandikishwa kabisa.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Muhamed Said, alisema katika bajeti inayopewa wizara, asilimia 20 ya fedha inakwenda katika sekta ya elimu. Alisema pamoja na kuwa haitoshelezi, mpaka sasa hakuna mwalimu aliekosa mshahara.

Alisema licha ya serikali kupitia katika kipindi kigumu cha maradhi ya UVIKO -19,  Rais Dk Mwinyi anasimamia wananchi kuhakikisha wanapata maendeleo. Kwa upande wao viongozi wa Jimbo la kwahani akiwemo, Mwakilishi Yahya Rashid Abdalla na Mbunge Ahmada Yahya Abdulwakil waliwapongeza waliochangia ujenzi wa madarasa hayo ambayo ni matunda ya mapinduzi katika miaka hii ya 58.

Walisema wilaya ya Mjini inakabiliwa na changamoto kubwa ya wingi wa wanafunzi madarasani hali inayopelekea kuwa na upungufu wa vyumba vya kusomea.

"Nikuombe Muheshimiwa Rais Dk Mwinyi utujengee Shule ya horofa katika eneo hili ambalo zitahudumia wananfuzi zaidi ya 100 kwa wakati mmoja lakini pia tutapunguza matumizi ya ardhi"alisema Ahmada  Yahya Mbunge wa jimbo hilo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE
JUMAMOSI JANUARI 8, 2022



DAVIDO HIYO NI JEURI YA FEDHA Uk.14



## ROSA REE

# Rapa anayewachanganya Wamarekani

RAPA Rosa Ree, ameweza kujiweka nafasi ya juu nchini Marekani, baada ya ushiriki wake katika kipindi cha 90 Day Fiance, kuwa kivutio.

Kipindi cha 90Day Fiance, kinarushwa kupitia kituo cha televisheni cha TLC nchini Marekani.

Kipindi hicho hufuatilia wapenzi ambao wameomba K-1 Visa, ambayo inatolewa kwa mtu ambae sio raia wa Marekani ambae yuko kwenye uhusiano na mtu wa taifa hilo.

Endapo ukifuata masharti yao ndani ya siku 90, basi unaweza ukawa na uhalali wa kuwa na uraia wa Marekani.

K- 1 Visa inagharimu kiasi cha Dola za Marekani 2025, sawa na shiligi 4, 673,700 na ukipata hiyo ndio itakupa uhalali wa kuishi Marekani na mwenza wako.

Katika msimu wa pili wa kipindi cha 90 Day Fiance, walikuja Tanzania kwa ajili ya kurekodi vipindi vyao na Rosa Ree ameonekana kushiriki.

Msanii huyo nyota yake inaonekana kuzidi kung'aa baada ya raia wa Marekani wengi kuvutiwa sana na ushiriki wake katika kipindi hicho huku wakitamani aendelee kuwepo.

BASI SAWA

## Profesa Jay usifurahie unaweza kurudi mjengoni

MWANAMUZIKI mkongwe na aliyekuwa mbunge wa Mikumi, Prof Jay, ni kama amefurahia kiaina kitendo cha kujiuzulu kwa Spika wa Bunge, Job Ndugai.
Baada ya kutolewa tangazo hilo, Profesa Jay, alitupia haraka video ya wimbo 'Nang'atuka' kwenye mtandao wa Instagram, huku akisema ni maalumu kwa Ndugai.
"TBT ya kibabe 'Nang'atuka', maalumu kwa Bwana Ndugai". Ameandika.




## Tantine aanza mwaka na hii



MWIMBAJI anayekuja kwa kasi kwenye muziki wa Injili, Tantine Esther, amewaomba mashabiki wa muziki huo kuipokea video ya wimbo wake mpya, Bwana Ndiye Mchunagaji.
Akizungumza na BT jana, Tantine alisema anashukuru mapokezi yamekuwa makubwa huku watu wakibarikiwa na ujumbe wa wimbo huo mzuri.
"Nimefungua mwaka na wimbo huo ambao umefanyika baraka kwa wengi, video imetoka Ijumaa na tayari ipo kwenye chaneli yangu ya YouTube hivyo naomba zaidi sapoti ili tuzidi kumtukuza Mungu pamoja," alisema Tantine.



# Joh Makini, Sallam SK vita imenza

SASA imekuwa mnyukano kati ya rapa Joh Makini na Meneja wa WCB, Sallam SK, baada ya wawili hao kuingia katika bifu kali kutokana na wimbo Don't Bother aliouimba msanii huyo.
Chanzo kilikuwa Sallam SK, ambaye alidai wimbo huo yeye alikuwa kiunganishi muhimu kati ya Joh Makini na AKA wa Afrika Kusini.
Hata hivyo, rapa huyo ameku-ja juu akisema Sallam anadanganya umma kwani yeye ndiye alipambana sana kukwamisha wimbo huo usifanyike.
"Aelezee aliunganisha vipi yeye sio chanzo cha hiyo collabo, kwa mazingira niliyofanya collabo na AKA nitawashukuru sana Nikki wa Pili na G NakoWarawara lakini waliomleta walikua hawataki itokee".
Ameongeza "Alipambana sana kukwamisha, hii basi tu Mwenyezi Mungu hajawahi kushindwa"





# Huu ndio ushauri wa Ommy Dimpoz

MSANII mkali wa Bongo Fleva, Omary Nyembo maarufu kama Ommy Dimpoz' ameanza mwaka kwa kuwashauri watu wasikate tamaa katika maisha.
Ujumbe huo ambao ameandika kwenye page yake ya Instagram unaeleza kuwa hakuna elimu ya maisha bali inatakiwa nidhamu na juhudi.
"Muhimu ni kupambania ndoto zetu, hakuna aliyesomea maisha, ukiwa na nidhamu na juhudi huku ukimuomba Mungu basi jua wakati wako utafika na riziki yako itaongezeka wala tusioneane choyo pale mwenzako anapopiga hatua". Ameandika.




# Ngoma 5 kali za dansi mwaka mpya

**Na Adam Fungamwango**

MWAKA mpya wa 2022 ndiyo kwanza umeanza . Kama tulivyoendelea kusema na tunavyoendelea kuandika kuwa muziki wa dansi ndiyo muziki pekee ambao hauachi kitu chochote kwenye jamii bila kutungia wimbo.
Unapotokea msiba, asilimia kubwa ya nyimbo zenye maudhui ya aina hiyo unakuwa ni muziki wa dansi. Yakitokea maafa yoyote nchini, nyimbo nyingi za maombolezo huwa ni za dansi na hata sikukuu za kiserikali mara nyingi, nyimbo kama za Muungano, Uhuru wa Tanganyika (sasa Tanzania Bara) huwa ni za muziki wa dansi.
Zikija sikukuu za kidini iwe Idd El Fitri au Krismasi, nyimbo zinazotamba ni za muziki wa dansi tu. Hata mwaka mpya pia, huwezi kukuta ngoma za bongo fleva zikizungumzia mambo ya mwaka mpya.
Tayari tumeingia mwaka mpya wa 2022. Kwa miaka mingi wanamuziki wa dansi wameendelea kuonyesha kuwa walikuwa bora zaidi, kwani wanazo nyimbo zinazozungumzia sikukuu ya mwaka mpya.

**1. Sikukuu Imefika-George Peter**

Ni wimbo ambao hutamba sana wakati wa Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya. Wimbo huu umetungwa na George Peter akiwa na bendi yake ya Jobiso, baada ya kutengana na kaka yake Wilson Peter Kinyonga kwa muda mfupi kabla ya kurejea tena Simba Wanyika.
Huu ndiyo wimbo maarufu zaidi wa Jobiso na baadhi ya watu hudhani ni wa Simba Wanyika.
Maudhui ya wimbo huu yanasema kuwa Sikukuu ya Krismasi imefika na Mwaka mpya unafika, hivyo watu wote wapite salama.
Mtunzi anamuomba Mungu awalinde wote waliobaki, kwani wakati Sikukuu hizo zinafika wengine wako hospitali, wapo waliofungwa na wengine wamekufa, hivyo anamuomba waliobaki wote Mungu awasaidie uzima na afya. Mungu atusaidie uzima 2022.

**2. Tufurahi Mwaka Mpya-Hamza Kalala**

Ni wimbo ambao Hamza Kalala anawahimiza watu wote wafurahi na mwaka mpya, wale vizuri, wavae nguo mpya, wanywe soda na kucheza.
Anasema siku hizi kumaliza mwaka ni kazi ngumu kwa sababu ya matatizo na magonjwa mbalimbali yanayowakabili wanadamu.
Hata hivyo ukiusikiliza sana wimbo huu, Kalala amechukua maneno mengi kutoka kwa wimbo wenye maudhui hayo hayo ya 'Tufurahi Kumwaka Mpya' ambao awali ulipigwa kwenye miaka ya 1950 hadi 1960 na Jean Mwenda Bosco.

**3.Happy New Year-Mbaraka Mwinshehe**

Mbaraka Mwinshehe alitunga wimbo wa Sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya, akiwataka watu waende kwanza makanisani wakasali, lakini wakitoka huko wapitie kwenye muziki wa Volcano ambayo ni bendi aliyokuwa akiiongoza.

**4. Bonne Annee-King Kiki**

Ni wimbo maarufu sana nchini Tanzania, hasa kinapokaribia kipindi cha Sikukuu za Krismasi na Mwaka Mpya.
"Natoka wapi, tukacheze mchezo wa sasa Kamanyola oo, tutoke naye, nakuchukua wangu kipenzi mi waoo hoho.." Ni baadhi ya maneno yaliyomo kwenye wimbo huo yakiimbwa na Kikumbi Mwanza Mpango King Kiki.
"Ooo Bonane mama" Ni kiitikio cha wimbo huo, wakiwa na maana mwaka mpya.

**5. Mwaka Mpya-MK Group**


Kwenye miaka ya 90, bendi matata ilivyovuma kwa kipindi kifupi lakini ikitikisa anga la muziki wa Tanzania, MK Group wakiwa na Kasongo Mpinda, walitunga wimbo wa Krismasi na Mwaka Mpya ambao nao pia ulikuwa ni moja na nyimbo maarufu sana kipindi hiki cha Mwaka Mpya,

# Muuza Mkaa: Mkaa safi au mzuri?

**Na Adam Fungamwango**

LEO tutaiangalia filamu safi ya 'Muuza Mkaa' ambayo inaangalia mambo mbalimbali ya kijamii, ikiwemo ile dhana ya kuwepo kwa viumbe wasioonekana kwa macho ya kawaida, yaani majini.
Katika dunia hii, kitu kidogo kinaweza kutokea tu kwa bahati mbaya, lakini kikazusha mambo makubwa na ya kutisha kiasi cha kuogofya watu, kufarakanisha watu na mengine yanayofanana na hayo.
Imechezwa na baadhi ya wasanii kama kina Hawa Mkwizu, Kassim Samwinzo, Ester Modekai, Abdul Shariff, Nasra Juma, Ibrahim Ally na wengineo.
Inaanza kuonyesha muuza mkaa akiwa amelala usingizi. Alikuwa kwenye eneo lake la kazi. Ghafla akaja dada mmoja, akamwamsha. Lakini wapi. Alipoona Muuza Mkaa amelala fofofo, akamimina mkaa kwenye chombo chake, na akachukua pesa na kuiweka mkononi mwa muuzaji. Hapo hapo aliamka. Akaanza kumfokea kwa anaiba mkaa wake. Akamwambia mkaa aliochukua ni mwingi kuliko pesa aliyompa. Akawa analalamika kuwa siku nyingi anapata hasara, kumbe ni mwanamke huyo. Wakati amemshika mkono akibishana, mara akapita mpenzi wake anaitwa Joyce.
Alipoona vile alidhani kuwa wapo kwenye mambo ya mapenzi. Ukazuka ugomvi mkubwa sana kati ya Muuza Mkaa wa mpenzi wake Joyce. Muuza Mkaa alimtafuta yule dada ili akamueleze mpenzi wake kuwa wao siyo wapenzi, ila yalikuwa ni mambo ya kudaiana tu, lakini dada yule alikataa.
Kuna siku Joyce alikutana na yule dada aliyekuwa ameshikwa mkono na mpenzi wake, akamkoromea sana, lakini hakujibiwa kitu.
Shoga wa Joyce anajiwa na mwanamke mmoja ambaye anamtuma akamkanye shoga yake tabia ya kumkasirikia mpenzi wake na kusema yeye si mpenzi wa Muuza Mkaa. Lakini katika kuongea akawa anajigeuzageuza kuwa mtu wa ajabu, mara ama makucha makubwa, mara na macho makubwa kitu ambacho kilimtisha mwenzake.
Mwanamke huyo anakwenda kumhadithia Joyce na kumweleza kuwa yule msichana anayemtuhumu anatembea na mpenzi wake si binadamu wa kawaida, ila ni jini.
Joyce na mpenzi wake nao wanatokea kwa nyakati tofauti na staili ya kijini. Wote wanakutana sasa na kwenda kumuomba radhi mdada huyo ambaye ni jini.
Wanamkuta nyumbani kwake, lakini anashangaa kuwa hajawahi kwenda kununua mkaa, wala kukutana na mtu yoyote kati yao, hivyo anashangaa.
Kilichogundulika kuwa dada yule huwa anaingiwa na jini na kufanya mambo ambayo yeye hajui kama anafanya. Alifunga ndoa na jini mwanaume wakati akiwa usingizini bila yeye kujua na ndicho kinachomsumbua.







# Davido hiyo ni jeuri ya fedha

MWANAMUZIKI nyota wa Nigeria, David Adeleke, maarufu kama Davido, amepanga kuzindua nyumba yake mpya iliyoko katika kisiwa cha banana.

Kupitia ukurasa wake wa Twitter, Davido amesema baada ya kuinunua nyumba hiyo iliyopo katika kisiwa cha kifahari, sasa ni muda wa kuizindua rasmi.

"Ninazindua nyumba yangu leo (juzi) mungu awabariki wote," ameandika.



## Kanye West sasa umezidi

RAPA nyota wa Marekani, Kanye West, anaendelea kumrusha roho aliyekuwa mke wake Kim Kardashian, baada ya kuripotiwa anatoka kimapenzi na mwigizaji mmoja wa Hollywood.

Kulingana na mtandao wa Pagesix, Kanye ameonekana akiwa na mrembo huyo katika mitaa ya jiji la New York, huku wakifurahia maisha katika eneo moja la michezo akiwa na kundi la marafiki zao.

Imeelezwa wawili hao walikwenda katika mgahawa mmoja maarufu wa Carbone kwa ajili ya chakula cha jioni, huku kundi la wapiga picha maarufu kama paparazzi wakiwaandama kila mahali.

## Bobi Wine aachia 'Ogenda' akiisema serikali

MWANAMUZIKI  Bobi Wine kutoka Uganda ambaye pia ni Kiongozi Mkuu kambi ya upinzani, ameachia wimbo mpya ukimlenga Rais Yoweri Museveni.

Wimbo huo unaoitwa Ogenda, neno  linalomaanisha "Utaanguka" kama ujumbe kwa Rais Yoweri Museveni kutokana na madai ya kukiuka ahadi yake kuleta demokrasia nchini humo.

Bobi Wine ameiambia BBC kwamba alilazimika kufichua uhalifu uliofanywa chini ya utawala wa kiongozi huyo  na ndio sababu picha zilizotumika kwenye video ni zile za kutisha.





## Mwigizaji afufuka baada ya kufariki saa chache

WASANII wa filamu kutoka Nollywood, wamejikuta wakipata mshangao baada ya mwigizaji mwenzao kuripotiwa amekufa na baada ya masaa machache akafufuka.

Januari 5, mwaka huu taarifa ya mwigizaji  mkongwe Iyabo Oko ilitolewa na mtoto wake wa kike, akisema amefariki baada ya kuugua kwa muda mrefu akiwa kitandani.

Hata hivyo, baada ya saa chache kupita binti huyo alisambaza taarifa nyingine katika mitandao ya kijamii kwamba mama yake bado yuko hai na hakufa kama ilivyotaarifiwa awali.

## Duncan pole, Mungu atakusaidia

MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Duncan Mighty , amelazwa hospitali baada ya kunusurika katika ajali mbaya ya gari.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, Duncan ameandika kwamba katika ajali hiyo anamshukuru Mungu kwa kupata michubuko mwilini na yupo hospitali akipatiwa matibabu.

"Mungu awabariki nyote kwa maombi yenu, Januari 2 nilikuwa njiani kutoka Uyo, gari letu lilikuwa likielekea mtoni baada ya kugongwa na lori lilokuwa likiendeshwa mwendo kasi, hicho ndicho ninakikukumbuka," amesema Duncan.



MAKALA

# Vijana wasomi Kiswahili, Kifaransa mpo ...

## •Kazi za staha zanusuru wengi

**Mwandishi Wetu**




Wahitimu wa vyuo vikuu nchini ni sehemu ya kundi la vijana wanaosaka ajira. **PICHA: MTANDAO**

MWAKA 2022 ni wa fursa kwa vijana, ni kwa sababu fursa za kufanyakazi kwenye mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), zinaelekea kufunguka.

Kinachowapa vijana nafasi hizo ni mkataba wa mabadilishano ya wafanyakazi vijana unaowawezesha kufanya kazi kwa muda maalumu pengine kuanzia miezi mitatu, sita na zaidi.

Anasema Nasibu Mwaifunga, Mratibu wa Masuala ya Kimataifa ya Uwezeshaji Vijana Kiuchumi kutoka Idara ya Maendeleo ya Vijana, Ofisi ya Waziri Mkuu, anabainisha hayo wakati anaelezea mikakati, sera na mipango inayofanywa na serikali kufanikisha ajira na kazi zenye staha.

Ni katika mkutano unaoandaliwa na shirika la ActionAid Tanzania, kujadili mradi wa kazi zenye staha kwa vijana, unaowaleta pamoja serikali, wadau wa ajira kutoka Bara na Zanzibar na vijana kutoka mikoa na sekta mbalimbali.

Anasema ii kuwanufaisha vijana serikali ilipitia sera kadhaa zinazohusika na ustawi wa wafanyakazi kwenye ajira ikiwamo sera ya ajira na ya mifuko ya hifadhi ya jamii.

Pamoja na hatua hiyo sera ya mabadilishano ya wafanyakazi vijana baina ya wanachama wa EAC, iliangaziwa upya.

Anasema sera hiyo itawahusisha vijana wa Afrika Mashariki na utekelezaji wake utaanza baada ya kukamilisha makubaliano na katika hatua za mwanzo sera hiyo imepitiwa na mawaziri na wataalamu.

"Katika protokali ya mkataba wa Afrika Mashariki kuna kipengele cha 'free movement of labour au kuruhusu wafanyakazi waanze kufanyakazi popote katika nchi wanachama. Tanzania tunachosema ni hiki ni lazima ziwe ajira rasmi hao ndiyo wanaweza kuajiriwa ndani ya jumuiya, " anasema.

Anasema mchakato utakapokamilika hati za makubaliano zitasainiwa (MOU) na katika

mabadilishano hayo, vijana wenye chini ya miaka 35, watafanyakazi ndani ya jumuiya ili kupata uzoefu na ujuzi unaowawezesha kuingia kwenye soko la ajira.

### BURUNDI NA TANZANIA

Tanzania na Burundi zina tume ya pamoja ya kudumu ya ushirikiano na wanashirikiana kwenye sekta karibu zote kama viwanda, biashara, miundombinu, anasema Mwaifunga.

"Wapo Watanzania wanaowekeza Burundi, kibiashara CRDB ina matawi Burundi, shirika la ndege lina safari Bujumbura. Burundi inatumia bandari zetu. Tumeona tushirikiane pia kwenye masuala ya kubadilishana wafanyakazi vijana. Tumekubaliana wanatuletea walimu wa Kifaransa tunawapelekea wa Kiswahili, pia Wakiingereza nao wanatuletea wa Kifaransa" Anasema Mwaifunga.

"Vijana wa Burundi watakuja na Watanzania watakwenda Burundi lengo ni kuwajengea uwezo na wale ambao hawana ajira lakini kuna nafasi kati ya nchi hizo wanaweza kuzipata kwa wenzetu. Tunaendelea na mazungumzo yakikamilika utekelezaji utaanza na Watanzania watajulishwa."

### USHIRIKIANO MISRI

Mwaifunga anasema Tanzania imesaini mkataba wa kushirikiana na Misri kwenye Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na maeneo ya kubadilishana vijana kwenye kujifunza utamaduni na michezo, lakini Tanzania inalenga zaidi TEHAMA ili vijana wajifunze na kuitumia kwenye fursa za uchumi.

Lengo ni kuwawezesha wazifikie fursa hizo na kujiingiza kwenye biashara mtandaoni -ecommerce, kutafuta masoko na kuuza mitandaoni.

### KAZI ZENYE STAHA

Mratibu wa Vijana, akizungumzia hatua zilizofikiwa kitaifa kufanikisha kazi zenye staha anapongeza juhudi za ActionAid, akisema ndiyo 'machampioni' wa kwanza wa kuwafahamisha Watanzania kuhusu kazi zenye staha.

Anasema vijana wengi na umma umefahamu kinachomaanishwa na kazi za staha kutokana na juhudi za shirika hilo za kuwafikia wafanyakazi, waajiri, maofisa kazi pamoja na kuzishirikisha serikali za pande zote.

Anataja hatua za karibuni kufanikisha mpango wa kazi zenye staha, akisema mwishoni mwa mwaka jana, Tanzania na Shirika la Kazi Duniani (ILO) walikutana kupitia na kufanya maboresho ya programu ya kitaifa ya kazi zenye staha.

Yaliyoboreshwa ni pamoja na kutengeneza ajira, hasa vijana, kuwaandaa kwa kuwapa ujuzi na uzoefu ili waajirike, anasema.

Mengine ni kuongeza vipengele vya masuala ya kanuni na haki za binadamu mahala pa kazi kwa kubainisha wajibu wa mwajiri, wafanyakazi na serikali.

"Kanuni na haki ni pamoja na kuhakikisha waajiriwa wanakuwa na mikataba, wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii, bima ya afya , wanalipwa fidia wakiumia kazini, haki ya likizo ya mwaka, uzazi na stahili zote kwa mujibu wa sheria za taifa na kimataifa ili kulinda utu wa watu na kukomesha vitendo vya unyanyasaji,"anasema Mwaifunga.

### MAFANIKIO ZANZIBAR

Ofisa Kazi Mwandamizi, Rashid Hamis Othman, kutoka Ofisi ya Rais Zanzibar Kazi, Uchumi na Uwekezaji, anawaambia washiriki kuwa uwepo wa programu hiyo umeleta nguvu mpya kazini visiwani humo.

Wafanyakazi wameanza kufuatilia haki zao na kufika kwenye vyombo vya kutoa maamuzi kama kitengo cha kutatua migogoro kazini (DHU).

Tangu kuanza kwa mradi miaka mitatu iliyopita malalamiko ya wafanyakazi yanayofikishwa kwa maofisa kazi yanazidi kupungua, anasema.

"Kuanzia mwaka 2019 hadi 2020 Kamisheni ya Kazi ilipokea malalamiko 200 ya wafanyakazi wakilalamikia, kusitishwa kazi na kukiukwa mikataba, kutolipwa mishahara na kupunguzwa kwa sababu ya corona na waathirika wengi walikuwa ni wanawake."

Anasema hata hivyo malalamiko yamepungua kutokana na ActionAid kuwafanyia waajiri na waajiriwa uhamasishaji kwenye sheria ya ajira namba 11 ya mwaka 2005, Sheria ya Mahusiano Kazini namba 8 ya mwaka 2005 , ya Usalama na Afya Kazini (OSHA) ya 2005, Sheria ya Hifadhi ya Jamii 2005 na ile ya Fidia kwa Wafanyakazi Ajali na Magonjwa ya 2005.

Othman anasema waliopewa mafunzo ni pamoja na waajiri, wafanyakazi, vijana wanaotafuta na wanaofanya kazi, vyama vya wafanyakazi na maofisa kazi na jumuiya ya waajiri na taasisi nyingi za serikali.

Wafanyakazi wa hotelini, nyumbani, shuleni viwandani, sekta ya utalii, uvuvi na huduma ni miongoni mwa walionufaika.

"Baada ya elimu kuna mafanikio mfano wafanyakazi wa ndani na hotelini wamejiunga na chama chao cha CHODAW, karibu 40 wameongezeka kwa miaka mitatu idadi imeongezeka, wako zaidi ya 2,000 tofauti na zamani walikuwa hawajiungi na chama hicho."

Anasema kwa ujumla wengi wamefahamu kuwa kazi zenye staha kuwa ni ajira zenye viwango kwa mujibu wa sheria na mikataba ya kitaifa na kimataifa.

### MABADILIKO KILWA

Vijana wa Kilwa wanaozungumzia kazi za staha kwenye mkutano huo, wanasema wafanyakazi wa migahawani, hotelini, uvuvi na majangwa na viwanda vya chumvi ni miongoni mwa wanufaika.

Said Mkoba, mjumbe wa Jukwaa la Vijana Kilwa (KIYOD) anasema sheria za mikataba ni moja ya masuala waliyohamasishwa kuyaelewa, kujenga uelewa wa vijana kudai stahiki zao kama likizo, mishahara na kupinga kufukuzwa kazi kiholela na huduma muhimu kama migahawa, vyoo na maji.

MAKALA

## TULIKOTOKA, TULIKO & TUNAKOELEKEA...

# Vituko simu za mkononi zilipotinga Bongo

Na Adam Fungamwango

DUNIA inakwenda kasi sana, kwani hivi sasa ukiangalia watu wengi wana simu za mkononi za kisasa kabisa maarufu kama 'smart phone'.

Ni simu zenye kila kitu, na hazitofautiani kabisa na kompyuta, na kwa kiasi kikubwa zinafanya kazi ile ile.

Zinafanya kazi nyingi mno kuliko simu za mkononi ambazo zilikuwa za mwanzo kuingia nchini katikati ya miaka ya 1990 hadi mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Awali kabla ya simu za mkononi kuingia, mambo yalikuwa magumu mno, lakini kwa bahati nzuri hakuna aliyejua kuwa watu wako kwenye hali hiyo.

Mke akitaka kusafiri kwao, basi mume atalazimika kumpa nauli ya kwenda na ya kurudia, la sivyo basi atampa nauli ya kwenda, halafu baada ya muda atatuma kwa njia ya posta ambapo ilichukua muda wa kuanzia wiki moja hadi mwezi mpaka kufika kutegemea na umbali.

Mtu na mkewe wakiachana mmoja akisafiri hakukuwa tena na namna ya mawasiliano kujua kama mwenzake amefika hadi pale, watakapoandikiana barua, au simu ya mezani ambayo ni lazima itakuwa kwenye ofisi kubwa za serikali, na nyumba za watu wenye wadhifa tu.

Kama hakuna hilo, mke au mume akisafiri huwezi kujua kama amefika salama, mpaka arudi hata ikiwa ni mwezi mzima.

Ni tofauti na sasa, wanaweza kuwasiliana hata wakati yupo kwenye basi amefika wapi hadi anafika.

Na hulazimiki kumpa nauli ya kurudia kwa sababu unaweza kumtumia kwenye simu siku hiyo hiyo anayorudi.

Katikati ya miaka ya 1990, simu za mkononi zilianza kuingia nchini na ni watu wachache sana waliokuwa nazo.

Kulikuwa na kampuni mbili za simu kubwa kabisa ambazo zilikuwa za kwanza kufanya kazi hiyo nchini. Nazo ni Mobitel na Tritel. Vocha ikiisha unalazimika kwenda kwenye ofisi za kampuni yenyewe ukawekewe.

Hata hivyo walioweza kumiliki ni watu wachache sana na hasa wa kwenye maofisi makubwa.

Hata mwanzoni mwa miaka ya 2000, ambapo baadhi ya watu hata uswahilini walianza kumiliki, lakini bado kulikuwa na vituko vingi kutokana na uhaba watu wanaozimiliki.

Mtu mmoja aliniambia kuwa ukoo mzima alikuwa nayo yeye na kaka yake mkubwa tu. Sasa kwa sababu ni yeye na kaka yake tu, hana wa kumpigia, basi ilikuwa anamsumbua sana kumpigia mara kwa mara.

Ni tofauti na sasa unapigiwa hadi unakereka, kila muda simu inaita.




Mwingine akasema alikuwa na simu yake kubwa mwaka 2000 na 2001, pale mtaani walikuwa nazo wawili tu, basi walikuwa wakipigiana wenyewe kwa wenyewe hata kama hawana lolote la kuongea.

Simu zenyewe zilikuwa kubwa kama 'redio call', zikipewa majina mbalimbali kama vile 'mshindi', 'kitochi' 'jeneza', 'dole tupu', na 'twanga pepeta'. Ziliitwa hivyo kutokana na wanamuziki wengi wa bendi ya African Stars 'Twanga Pepeta', ambayo kwa wakati huo ilikuwa ndiyo inavuma mno, kuwa nazo, na walikuwa moja wa



**Mke akitaka kusafiri kwao, basi mume atalazimika kumpa nauli ya kwenda na ya kurudia, la sivyo basi atampa nauli ya kwenda, halafu baada ya muda atatuma kwa njia ya posta ambapo ilichukua muda wa kuanzia wiki moja hadi mwezi mpaka kufika kutegemea na umbali.**

watu wa mwanzo kumiliki simu za mkononi wakati huo.

Mbwembwe zao waliokuwa na simu wakati huo walikuwa wakizungumza kwa muda mrefu mno. Na wengine walikuwa waongo, walikuwa wanataka tu kuonekana wana simu za mkononi.

Halafu wengi kwa sababu walikuwa hawajazoea kuona watu wengi wana simu, unaweza kumkuta mtu amesimama karibu na jalala, anaongea kama peke yake hivi ukashtuka, kumbe anaongea na simu ya mkononi.

Vocha ziliitwa 'dola', kutokana na vocha ya kwenye simu kuhesabiwa kwa thamani ya dola ya Kimarekani. Ukiweka dola moja, basi itakulazimu kutoa Sh 5,000 ya Kitanzania, tofauti na sasa kuna vocha hadi za Sh. 500. Wakati huo hakuna hata kujiunga na kifurushi.

Kutokana na gharama kubwa sana ya kumiliki simu kukawa na vibanda vya mawakala kama hawa wa sasa wa kutuma pesa na wafanyabiashara waliokuwa wakitoa huduma za simu.

Hao walikuwa ni wa kupigisha simu. Ilikuwa ni balaa tupu, 'kubeep' tu ilikuwa Sh 500, wakati huo wengi uswahilini waliita 'kudipu'.

Acha na huduma hiyo kulikuwa na huduma ya kutumiana meseji, kupiga, na kupigiwa.

Jamaa mmoja aliniambia kijijini kwao walikuwa wanamlipa mwenye kibanda cha simu kwa kupokea simu yako tu kutoka mjini.

Siku ikipigwa kutoka mjini, anatafutwa aliyepigiwa kijiji kizima hadi apatikane na kwa kuwa walikuwa wanajua, basi haikuwa shida sana.

Mjini nako, unawekewa muda kwa mpigaji kwenye kibanda, halafu jamaa anakata muda ukiisha, inabidi uongeze tena pesa au uondoke tu.

Wakati huo pia hakukuwa na pesa za kwenye mtandao. Ni baada ya matumizi ya simu kupamba moto, watumiaji walianzisha ujanja wa kutumiana vocha kwenye simu, na anayetumiwa anafanya kazi ya kuuzia wenzake hadi kupata kiasi cha pesa alizotumia.

Mfano akitumiwa vocha ya sh 10,000, mtumiaji atauza vocha kwa wanaohitaji salio, iwe Sh. 1,000 au Sh 500, hadi yote iishe, ndipo anapata kiasi cha pesa alizotumiwa. Hiyo iliifanya Serikali na Kampuni za simu kuanzisha huduma hiyo ambayo kwa sasa inaipatia mapato na tozo kwa ajili ya maendeleo ya nchi.

HABARI KIMATAIFA

# Rais aamuru wanajeshi kupiga risasi

**ALMATY,** KAZAKHSTAN

KIONGOZI wa Kazakhstan, anayeiongoza nchi hiyo ameamuru vikosi vya usalama kufyatua risasi bila onyo wakati kunaendelea na msako mkali wa kuwadhibiti waandamanaji wanaopinga serikali.

Rais Kassym-Jomart Tokayev, alisema watu aliowaita majambazi 20,000 wameshambulia katika mji mkuu wa Almaty, ambako ni kitovu cha maandamano yaliyochochewa na ongezeko la bei ya mafuta.

Amewalaumu magaidi waliofunzwa kutoka nje, hata hivyo bila kutoa ushahidi.

Wizara ya Mambo ya Ndani ilisema wahalifu wenye silaha 26 na maofisa wa usalama 18 waliuawa kufikia jana katika machafuko hayo.

Katika hotuba yake kwa njia ya televisheni, Rais Tokayev, alisema vikosi vya kulinda amani vilivyotumwa kutoka Urusi na mataifa jirani vimefika kwa ombi lake na viko nchini kwa muda ili kuhakikisha usalama.

Kikosi kutoka kwa Jumuiya ya Mkataba wa Usalama wa Pamoja (CSTO) inayoongozwa na Urusi, kikiwa na wanajeshi 2,500 kiliwasili nchini humo.

Rais Tokayev alitoa shukrani maalumu kwa kiongozi mwenzake kutoka Urusi Vladimir Putin, kwa kutuma wanajeshi hao.

Mapema siku ya Ijumaa, milio mipya ya risasi ilisikika karibu na uwanja wa ndege wa Almaty. **BBC**

# Tukio la manowari ya kirusi kugonga meli ya kivita ya Uingereza lafichuliwa

**LONDON,** UINGEREZA

MANOWARI ya kijeshi ya Urusi imegongana na meli ya kivita ya Uingereza ilipokuwa katika doria kaskazini mwa bahari ya Atlantic.

Wizara ya Ulinzi ya Uingereza imethibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kueleza, meli hiyo inayoitwa HMS Northumberland, ilikuwa ikifuatilia manowari wakati ilipoigonga.

Katika ajali hiyo, kipande cha nyuma ya meli kilionekana kuning'inia.

Tukio hilo, lililotokea mwishoni mwa mwaka 2020, lilinaswa na wafanyakazi wa televisheni waliokuwa wakichukua picha za filamu kwa ajili ya makala.

Chanzo cha Ulinzi cha Uingereza kilisema kugongana huko hakukuwa kwa makusudi.

Meli hiyo ilikuwa ikisaka manowari katika uzio wa Arctic baada ya kutoweka kutoka kwenye mtambo wa ufuatiliaji wa safari za meli, kulingana na kituo cha habari cha Channel 5, ambacho kilikuwa kinachukua picha za filamu kwa ajili ya meli zake za kivita na msururu wa filamu za Life at Sea **BBC**.

# Mke apanga kushtaki polisi kumshikilia mume wake

**KAMPALA,** UGANDA

MKE wa mwandishi wa riwaya wa Uganda, Kakwenza Rukirabashaija, ambaye yuko kizuizini, ameanza mchakato wa kisheria dhidi ya wakuu wa polisi wa nchi hiyo ili kupata haki ya kumuona mumewe.

Eva Basima, alimshitaki Kamanda wa Kikosi Maalumu na Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP) akitaka kutoa ruhusa ya kukutana na mume wake.

Alisema hajafanikiwa kumuona mume wake , ambaye ni mkosoaji wa Rais Yoweri Museveni, tangu alipokamatwa na askari wa kikosi maalumu kilichojihami kwa silaha Desemba 28, mwaka huu akiwa nyumbani kwao.

Hata hivyo, Jumanne Mahakama iliamuru polisi kumwachilia Rukirabashaija bila masharti, lakini anaendelea kuzuiliwa.

Robert Kyagulanyi, Kiongozi wa Upinzani na mwimbaji wa muziki, Bobi Wine, alisema kushindwa kumwachia mwandishi huyo ni uhalifu dhidi ya binadamu.

Polisi wanamtuhumu Rukirabashaija kwa kutumia mitandao ya kijamii kumtusi na kumdharau rais na mwanawe, Kamanda wa Jeshi, Luteni Jenerali Muhoozi Kainerugaba. **BBC**



Wanajeshi kutoka Urusi wakiwa na gari la deraya wakilinda mitaa ya mji wa Almaty nchini Kazakhstan **PICHA: BBC**

# Ufunguo jela ya Mandela kurudishwa Afrika Kusini

**CAPE TOWN,** AFRIKA KUSINI

UFUNGUO seli ya gereza ya kisiwa cha Robben alikofungwa Nelson Mandela, hatimaye utarudishwa Afrika Kusini badala ya kupigwa mnada nchini Marekani.

Waziri wa Utamaduni wa Afrika Kusini, Nathi Mthethwa alipinga mnada mwingine ambao ulitakiwa kufanyika Januari 28 mwaka huu jijini New York.

"Ufunguo huu ni wa watu wa Afrika Kusini," alisema.

Mandela alitumikia kifungo cha miaka 27, wakati akipambana na utawala wa kibaguzi wa makaburu.

Miaka kumi na minane kati ya hiyo, alikuwa kwenye kisiwa cha Robben, karibu na Cape Town.

Mwaka 1994, alichaguliwa kuwa rais wa kwanza mweusi wa Afrika Kusini katika uchaguzi wa kwanza wa kidemokrasia nchini humo.

Waziri Mthethwa alisema jumba la mnada la Guernsey lilikubali kurudisha ufunguo huo nchini humo na pia kusitisha uuzaji wa vitu vingine vilivyokuwa vya Mandela.

Vitu hivyo ni pamoja na mchoro asilia wa Mandela 'The Lighthouse' , Robben Island, pamoja na baiskeli ya mazoezi aliyoruhusiwa kutumia na raketi ya tenisi gerezani

"Ufunguo unaashiria historia chungu ya Afrika Kusini, huku pia ikiwakilisha ushindi wa roho ya mwanadamu dhidi ya uovu," alisema Mthethwa.

Ufunguo huo ulikuwa umeuzwa na Christo Brand, mlinzi wa zamani wa jela hiyo yenye sifa mbaya. Wawili hao walikuwa marafiki wa karibu.


Mnada huo ulikuwa wa kuchangisha fedha kwa ajili ya bustani ya kumbukumbu na makumbusho karibu na eneo la maziko ya Mandela.

Mandela aliachiliwa kutoka gerezani mwaka wa 1990 wakati Afrika Kusini ilianza kuachana na ubaguzi mkali wa rangi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



**KUBULI HAMISI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1728-0022 kilichototolewa Baraza na Mitihani la Taifa kupitia **RASHIDI MFAUME KAWAWA SEKONDARI** mwaka 2008. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **LIN/LIW/RB/611529/2021.**

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na. 17/2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU OMARY SHOMARY MUMBA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA SAID OMARY MUMBA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 Mwezi 01 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 5 Mwezi 01 Mwaka 2022.

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
KITUO JUMUISHI
HUDUMA ZA KIMAHAKAMA
MIRATHI NA NDOA
DAR ES SALAAM

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MPANDA AT MPANDA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 1 2022**
**in the Matter of the Estate of the Late PATRICK**

**MTANDULA RICHARD and in the Matter of Application for ADMINISTRATION By ADROPHINA EDWARD SIZYA.**
**FORM 58**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75)**

All person claiming to have any interest in the estste of above – named deceased are herby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above –named petitioner.

Objections to **the grant shoulbe filed on or before the 21RD day of JANUARY, 2022 Dated 3RD day of JANUARY2022**

RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
MPANDA - KATAVI

**RESIDENT MAGISTRATE**

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na. 2/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MUHUNZI RASHID ISMAIL**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MWANAHAMISI IBRAHIM na ISMAIL RAJABU TUNGU**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 25 Mwezi 01 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imetolewa leo tarehe 3 Mwezi 01 Mwaka 2022.**

HUDUMA ZA KIMAHAKAMA
MIRATHI NA NDOA
DAR ES SALAAM

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

REGINALD MATHEW MASSAWE anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili MC 244 CCS – TVS STAR. Chassis namba MD625AF79JILA2410. Engine namba AF7LJ10A2652. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: DAR/MBU/RB/9435/2022.

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

MARIANE CHARLES SHUMA ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA PASSO YENYE NAMBA ZA USAJILI T 917 CNV KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAH/TR/RB/ 17/2022

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**
**Usimamizi wa mirathi Na 82/2021**
**Ignas Dickson Pella::::::::::::::::::::::::::Marehemu**
**Vestina Joseph Mlelwa::::::::::::::::::::::Msimamizi**
**TAARIFA KWA UMMA**
**MAOMBI YA KUFUNGA MIRATHI**

Kwa wote wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi.
Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 05 ya mwezi wa Februari,mwaka 2022.
Imetolewa na Hakimu Mkazi leo siku ya tarehe 05, Januari, mwaka 2022.

..............................
**HAKIMU MKAZI**
**NJOMBE**

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

DIANA ni msichana mrembo kwa maana halisi ya urembo. Na mwenyewe alijijua kuwa ni mzuri wa shani. Aliwababaisha, kuwaliza na kuwatia wazimu wanaume wengi ambao walikutana nao, au hata kupishana tu. Wengi walimkimbilia. Wakamtongoza, kumtaka kimapenzi. Wapo waliotaka kumuoa kabisa. Hata hivyo yeye mwenyewe hakujua ni mwanaume gani anayempenda kwa dhati. Alichojua wengi wanamfuata kama nyuki wafuatavyo ua zuri la waridi. Aliacha muda uongee. Alijua mwisho wa siku atajulikana ni nani anayependa uzuri na urembo wake na nani nampenda kwa dhati. Alayempenda yeye kama yeye na si urembo wake. Fuatilia mtiririko huu wa riwaya hii kabambe, yenye kusisimua na mafunzo kwa jamii.

# Operesheni Namba Moja-8

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

“Usikasirike, mimi nimekwambia hivyo nina maana yangu. Sikutaka kukuficha chochote kile. Nilikuwa na uwezo wa kusema sina mtu yoyote na ningeweza kukuficha kwa kipindi ambacho mimi nahitaji nikufiche.” Diana alimpoza Jan na yalikuwa ni maneno ambayo angalau yalionekana kumfariji na akili yake inaanza kurudi.

“Una maana gani kusema hivyo?”

“Ni hivi mpenzi. Siyo kosa langu ni Mungu amepanga hivi, sina uwezo wa kutengua. Ningeanza kukutana na wewe, hawa wawili nisingekuwa nao. Lakini nilikutana na mwanaume mmoja mfanyabiashara anaitwa Chala katika mazingira ambayo mimi sikuwa na mpenzi yoyote, achana na hawa wanaonifuatafuata. Halafu huyu mwingine ni askari, nilimpata nilipopata ajali ya bodaboda. Kwa bahati mbaya wewe nimekupata mwishoni. Na wewe ndiye nakupenda zaidi yao.”

Jan na Diana walikuwa kwenye hoteli moja Kinondoni Mkwajuni, Dar es Salaam, ambapo waliamua kukaa hapo kutwa nzima kwa ajili ya kufahamiana zaidi, Diana akilipia gharama zote.

“Unasikia Jan, mimi nakuhitaji wewe na sitaki upate matatizo, kwa hiyo hili suala la hawa wawili niachie mimi, ila sitaki uwe na wivu kwa hivi sasa.

Najua huko mbele ya safari nini nitafanya ili tubaki mimi na wewe. Nikisema eti leo nimekupata wewe, halafu niachane nao ghafla, kama nilivyokwambia mmoja ni mfanyabiashara mkubwa ana pesa balaa, anaweza kuweka wapelelezi na kujua ni kwa nini nimeamua kumuacha, akijua kuwa ni wewe, ndugu yangu umekwisha, anaweza kukuua kwa mbinu yoyote ile.”

Ni maneno ya Diana kuelekea kwa Jan, ambaye sasa aliamua kukaa kimya na kukubali matokeo.

Ni kweli hakuwa na uwezo kipesa, wala cheo kuliko hao. Pia ndiyo alioanza nao. Yeye ajione tu mwenye bahati ya kukubaliwa na msichana mrembo.

“Jan, usiwe mnyonge, jione ni mshindi kwa sababu umewashinda wote. Sikuwa na sababu tena ya kuwa na mwanaume mwingine, lakini nimekukubali wewe. Umewapiku wao, usiwe na wasiwasi.” Alisema akimpetipeti.




**“Hawa siyo watu wa kuwatema hivi hivi ghafla, wananipenda hatari, sasa wakijua kuwa tatizo ni wewe, mtoto wa watu nitakuwa nimekuweka kwenye hatari. Na mimi sitajisamehe kwa hili.” Alikumbuka Diana akimwambia.**

“Ila ninachokuomba ikitokea siku yoyote ile ukiona nipo na mmoja wapo. Basi wewe nitakutambulisha au ujitambulishe kuwa ni mdogo wa mjomba wangu. Yaani ni mdogo wa mjomba wangu kuanzia leo, hadi hapo malengo yangu yatakapokamilika, sawa? Diana alimwambia kwa upole na upendo, lakini akionekana kumaanisha kile anachokisema.

****************************

Ni wiki mbili zimepita. Jana alikuwa ofisini mwake akitengeneza moja ya pikipiki alizoletewa. Mawazo yalimpeleka wiki moja nyuma. Akakumbuka alipoitwa tena mpenzi wake Diana. Alikwenda na pikipiki yake kubwa. Baada ya pale anampeleka moja kwa moja hadi kwa Chala. Akamtambulisha kuwa ni mjomba wake, ni mdogo wa mjomba ambaye anaishi kwake.

Wakapewa shilingi laki mbili. Kila mtu akachukua laki moja.

Baada ya kutoka hapo alikwenda naye hadi kwenye kituo cha Polisi Ubungo kwa afande Marco. Hapo napo akatambulishwa hivyo hivyo. Mbali na kununuliwa chakula cha mchana, lakini walipewa shilingi elfu hamsini ambayo yote Diana alimkabidhi Jan baada ya kuondoka.

“Unaona? Hawa wanajigonga tu kwangu, wala usiwe na wasiwasi. Na nadhani umeshaelewa kama mimi nakupenda. Ningekuwa sikupendi wala nisingekuwa na haja ya kukupelekwa kwao na kukutambulisha. Nimefanya hivi ili hata siku moja wakituona mimi na wewe kwa bahati mbaya, basi wasiwe na wasiwasi. Najua vinginevyo wewe ndiyo ungekuwa kwenye hatari zaidi.”

Yalikuwa ni maneno ya Diana akiwa yupo nyuma ya pikipiki, akiwa amemshikilia kiunoni Jan.

“Mwanzoni sikukuelewa baby, lakini kwa sasa nimekuelewa.”

“Hawa siyo watu wa kuwatema hivi hivi ghafla, wananipenda hatari, sasa wakijua kuwa tatizo ni wewe, mtoto wa watu nitakuwa nimekuweka kwenye hatari. Na mimi sitajisamehe kwa hili.” Alikumbuka Diana akimwambia.

**********************************

Taarifa ya habari ya televisheni ya saa mbili usiku ilitangaza moja ya tukio moja la kusikitisha lililotokea jijini Dar es Salaam.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Kinondoni Bernard Chipeta alitangaza kutekwa kwa mwanamke mmoja mwenye umri wa miaka 25 aitwaye Diana Khan na watu wasiojulikana.

Kamanda akasema kwa mujibu wa mashuhuda ni kwamba, Diana alikuwa kwenye bodaboda moja ambayo aliipanda maeneo ya Makumbusho iliyokuwa impeleke Ubungo, lakini ilipofika eneo la Mwenge ilikutana na bodaboda zingine mbili ambazo zilimzuia njia na ilibidi asimame.

“Wakati huo huo gari moja lilikuwa nyuma likafika, halafu watu wawili walishuka na kumbeba kutoka kwenye kiti cha bodaboda na kumuingiza ndani ya gari hilo, wakaondoka. Haikupigwa risasi yoyote ya kutisha watu wala hawakutumia nguvu kubwa. Walikuwa ni kama watu waliojipanga hivi. Na wakafanikiwa kufanya walichokifanya. Tunawaambia wananchi wote, yoyote yule atakayemuona Diana, au kuona watu hao, au kuwahisi atoe taarifa upesi kwenye Jeshi la Polisi na upande wetu tayari uchunguzi umeshaanza.” Alisema Kamanda huyo.

Jan ni mmoja kati ya watu walioona habari hiyo. Wakati wengine waliona kama habari kama zingine tu za kusikitisha, yeye ilikuwa zaidi.

Aliyetekwa ni mpenzi wake. Hakuamini kile kilichokuwa kikizungumzwa. Anakumbuka kabla ya kutekwa majira ya saa 10:00 jioni, mchana walizungumza kwenye simu akiwa ofisini.

“Wamemteka kwa sababu gani? Amefanya nini mtoto wa watu?” Alijiuliza machozi yakiwa yanamtoka.

Alikuwa anaiangalia taarifa hiyo ya habari akiwa chumbani kwake peke yake.

“Au ni wale wale ambao ameniambia ni wapenzi wake? Inawezekana mmoja wapo amegundua hili, ameamua kumteka kwa ajili ya kumtesa ili aachane na mimi.” Aliwaza.

Nguvu zilimuishia. Alilia kwa muda mrefu. Usingizi hakuupata. Akili ikamtuma kuwa kesho yake asubuhi atoke na kwenda Ubungo kwa mjomba wake anakoishi ili yeye na familia ya Diana kuona ni jinsi gani wanaweza kushirikiana na polisi kuhusu jambo hili.

******************************

“Karibu kijana.”

“Ahsante Mjomba.”

“Kama ulivyosikia, Diana ametekwa.” Ilikuwa ni sauti ya upole ya mjomba wake Diana.

“Ndiyo mjomba, ndiyo maana nimekuja tujue nini tutafanya.”

“Jana usiku wa manane, wakati sijui ni nani amemteka au kwa sababu gani. Kuna meseji imeingia kuwa hawa watekaji wanahitaji kiasi cha shilingi milioni hamsini ili wamuachie.

Jan alishtuka. “Milioni hamsini?”

“Ndiyo na wamesema nisilipeleke suala hili polisi na wao wana mtandao mpana sana, nikienda tu kuwaambia polisi watamuua mara moja. Kwa hiyo hapa sijui nifanye nini. Bora umekuja mjomba tushauriane.”

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

HABARI MICHEZO

# AZAM FC, YOSSO BOYS KUKAMILISHA RATIBA LEO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Azam FC kutoka jijini Dar es Salaam inatarajia kukutana na wenyeji Yosso Boys katika mechi ya kukamilisha ratiba ya Kundi A ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan visiwani hapa.

**Azam itashuka dimbani tayari ikiwa imeshatinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo baada ya kushinda mechi zake mbili za awali wakati Yosso Boys yenyewe haina pointi hata moja.**

Matajiri hao wa Chamazi watasubiri kujua wanacheza na nani baada ya kukamilika kwa mechi ya jana usiku kati ya vinara wa Ligi Kuu Bara, Yanga dhidi ya 'Maafande' wa KMKM. Timu nyingine kutoka Kundi A ambayo imesonga mbele katika michuano hiyo ni Namungo FC, ambayo nayo imemaliza hatua hiyo ya makundi ikiwa na alama sita kibindoni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Azam FC, Abdulhimid Mohamed, alisema amefurahi kuona malengo yake ya kusonga mbele katika michuano hiyo yametimia na sasa kilichobakia ni kuhakikisha anatinga fainali na hatimaye kuchukua ubingwa. Kocha huyo alisema mechi zote za mashindano hayo ni ngumu na zina ushindani, hivyo anawajenga wachezaji wake kupambana bila kukata tamaa dakika zote 90 za mchezo.

"Ingawa tumeshatinga hatua ya nusu fainali, bado tunahitaji kupata alama tatu ili kuliongoza kundi hili, tunawaheshimu wapinzani wetu Yosso boys, kutosonga mbele kwao haina maana timu hiyo sio bora," alisema kocha huyo.

Aliongeza kila timu imeingia kwenye michuano hiyo ikiwa na malengo yake hivyo wamejipanga kukabiliana na ushindani kwa timu yoyote watakayokutana nayo kwenye hatua ya nusu fainali.

"Tumekuja Zanzibar kufuata kombe hili, sisi ndio mabingwa wa kihistoria wa michuano hii, tumejipanga na malengo yetu ni kushinda kila mechi iliyoko mbele yetu," alisema Ofisa Habari wa timu hiyo, Zakaria Thabit.

Naye Kocha Mkuu wa Yosso Boys, Abdulrahman Talib, alisema licha ya kuwa tayari kikosi chake kimeshaondolewa katika michuano hiyo, anahitaji kushinda mchezo huo wa mwisho ambao ni wa kukamilisha ratiba ya hatua ya makundi.

"Nahitaji kupata alama tatu japo hazitonipeleka sehemu yoyote, haimaanishi kutupwa nje ya mashindano basi mchezo wa kukamilisha ratiba tusicheze kwa kujituma, tunahitaji tuage mashindano haya walau kwa alama tatu, kwetu itakuwa heshima pia," alisema kocha huyo.

Alisema ushindani wa kuwania namba kwenye kikosi chake umeongeza umakini wa wachezaji ambao wanahitaji kupata nafasi ya baada ya kurejea katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

## *Simba SC yaihofia Azam Mapinduzi*

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba wamesema wanaihofia Azam FC pekee kwa sababu ndiyo timu inayobadilika na kuwa 'moto' kila inaposhiriki katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayofanyika Zanzibar.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema mara nyingi Azam inapokuwa kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi inakuwa tofauti na ile iliyozoeleka kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

"Michuano ya mwaka huu imeongezeka mvuto na ugumu, ukiziangalia timu za Azam na Namungo zimebadilika, hasa Azam wakiwa huku kwenye michuano hii wanakuwa hatari sana, labda wanajihisi kama wapo nyumbani, kwa hiyo kidogo tunakuwa na wasiwasi nayo, lakini siyo kama hatuwezi kuwafunga, ila tutakuwa makini kama tukicheza nao," alisema Ally.

Alisema kuwa hana wasiwasi na kikosi cha Simba kwenye michuano hiyo, na kitakachofanyika sasa ni kunoa safu ya ushambuliaji mbele ili kutumia nafasi nyingi zinazopatikana.

Aliongeza timu yao bado inaendelea kujiimarisha zaidi katika eneo la ushambuliaji huku akikiri safu yao ya ulinzi iko vizuri.

Aliwataka wanachama na mashabiki wao kuwaunga mkono wachezaji kwa kujitokeza kwa wingi viwanjani popote pale wanapokwenda ili kuwaongezea morali.



Wachezaji wa Timu ya Soka ya Taifa ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), wakifanya mazoezi kujiandaa na mashindano ya kimataifa yatakayofanyika Uturuki kuanzia Januari 15, mwaka huu. Serengeti Boys ni mwalikwa katika michuano hiyo. **PICHA: TFF**

## Yanga yabeza majaribio Simba

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Yanga imewatupia 'dongo' watani zao Simba kutokana na uamuzi wa kutumia wachezaji wa majaribio katika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea Zanzibar na kusema ni kuikosea heshima michuano hiyo.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema uamuzi uliofanywa na Simba si mzuri kutokana na ukubwa wa michuano hiyo.

"Umeshawahi kuona Manchester United inampeleka mchezaji kwenye michuano fulani kumfanyia majaribio? Klabu ndogo ndiyo zina tabia ya kujaribisha wachezaji, sisi Yanga tumeshavuka huko. Wachezaji wote tunaowatumiwa tumewasajili kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema Bumbuli.

Baadhi ya wachezaji ambao Simba imetangaza inawafanyia majaribio ni pamoja na Sharaff Eldin Shiboub kutoka Sudan na Cheik Moukoro raia wa Ivory Coast.

Kuhusu michuano hiyo, Bumbuli alisema timu yao ilipangwa katika kundi gumu kwa kucheza dhidi ya klabu zilizo kwenye vita ya kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Zanzibar tofauti na wapinzani wao.

## Julio akasirika kuikosa Yanga

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio' amesema alitamani kukutana na Yanga katika hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi yanayoendelea visiwani hapa kwa sababu 'anawamudu'.

Namungo iliambulia kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Azam na hivyo kumaliza hatua ya makundi ikiwa katika nafasi ya pili, hivyo inasubiri mshindi kati ya Simba na Mlandege ambao walitarajia kukutana jana usiku.

Akizungumza na gazeti hili jana, Julio alisema katika mchezo wao dhidi ya Azam walipaswa kucheza kwa nguvu ili kuwafunga lakini hali ilikuwa ni tofauti na matarajio yao.

"Hesabu zetu zilikuwa ni kukutana na Yanga kwenye hatua ya nusu fainali halafu Simba tungecheza nao fainali, sijafurahia ratiba ilivyokaa sasa," Julio alisema.

Aliongeza kwa kuwapongeza wachezaji wake kwa kupambana katika mchezo huo licha ya kupoteza pointi zote tatu.

## ZISIKUPITE

### RONALDO KUONDOKA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo, 36, huenda akaondoka Manchester United msimu huu wa joto ikiwa hataridhika na chaguo la klabu hiyo la kocha wa kudumu. ***(Star)***

### DIAZ KUTUA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanakaribia kufikia mkataba wa kima cha pauni milioni 60 kumsajili winga wa Timu ya Taifa ya Colombia, Luis Diaz, 24, kutoka Porto. ***(Sun)***

### ORIGI HUYO NEWCASTLE

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Mbelgiji Divock Origi, 26 na straika wa Bournemouth (24), Dominic Solanke ni miongoni mwa wachezaji wanaonyatiwa na Newcastle United ambao wanatafutwa kujaza pengo lililoachwa na Callum Wilson aliyejeruhiwa. ***(Telegraph)***

### LONGSTAFF AZUIWA

KLABU ya Newcastle wamekataa dau la Everton la kumnunua, Sean Longstaff, 24. Mkataba wa kiungo huyo unakamilika mwisho wa msimu huu. ***(Shields Gazzette)***

### CANTWELL AGEUKA LULU

NEWCASTLE United na klabu nyingine za Ligi Kuu England zinapania kumsajili kiungo wa kati wa Norwich, Todd Cantwell, 23. ***(Sky Sports)***

### POCHETTINO AIOTA UNITED

KOCHA wa Paris St-Germain, Mauricio Pochettino yuko tayari kupokea ofa yoyote ya kuwa kocha mpya wa Manchester United. ***(Sun)***

### COUTINHO ATUA VILLA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Philippe Coutinho, 29, ametangazwa rasmi kutua Aston Villa kutoka Barcelona huku uamuzi kuhusu hatima ya Mbrazili huyo ilitarajiwa kutolewa jana Ijumaa. ***(Sky Sports)***

### SPURS YAMTAKA TRAORE

KLABU ya Tottenham Hotspur ipo tayari kufufua mpango mpya wa kumsaka winga wa Timu ya Taifa ya Hispania na Wolves, Adama Traore, 25. ***(Athletic)***

### CHELSEA YAMGOMEA NIGUEZ

CHELSEA haiko tayari kulipa ada inayohitajika kumfanya kiungo wa kati anayecheza kwa mkopo, Saul Niguez, 27, kusajiliwa mkataba wa kudumu Atletico Madrid. ***(Express)***

### RICE ATAJWA UNITED

KLABU ya Manchester United haina mpango wa kufanya usajili wowote mwezi huu, lakini watamtafuta kiungo wa kati msimu wa joto, huku mchezaji wa kimataifa wa England, Declan Rice, 22, akitajwa kuwaniwa. ***(Sport)***

### PHILLIPS NJIA NYEUPE

KLABU ya Watford imewasilisha ombi la kutaka kumnunua beki wa kati wa Liverpool, Nathaniel Phillips, 24, ambaye ameambiwa anaweza kuondoka kwa wekundu hao mwezi huu. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBIO ZA KUMNASA HAALAND ZAKOLEA

**Chelsea nayo yaonyesha nia ya kumwania mshambuliaji huyo baada ya...**

**LONDON,** England

BAADA ya Romelu Lukaku kuleta sintofahamu, Chelsea wameripotiwa kurejea kwenye mbio za kumsajili mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland.

Lukaku mwenye umri wa miaka 28, hivi majuzi aliomba msamaha hadharani kwa mashabiki wa Chelsea baada ya mahojiano na Sky Sport Italia.

**Staa huyo alinukuliwa akisema hakufurahishwa na hali yake pale Stamford Bridge na alikuwa na nia ya kurejea Inter Milan siku za usoni, ikiwa ni miezi mitano tu baada ya uhamisho wake wa pauni milioni 97.5 kutua hapo Blues.**

Kwa mujibu wa Bild, mzozo wa Chelsea na Lukaku unaweza kubadili msimamo wao wa kumsaini Haaland msimu ujao wa joto, ambapo hawakumfikiria kuwa lengo kuu.

Ripoti hiyo inaongeza mazungumzo ya Lukaku na Thomas Tuchel nyuma ya pazia hayajaenda vyema sana, huku kocha huyo raia wa Ujerumani akiona matamshi ya Mbelgiji huyo kama tusi kwake.

Haaland anatarajiwa kuwa mmoja wa washambuliaji wanaotafutwa sana duniani katika majira ya joto wakati kifungu chake cha kuachiliwa kwa pauni milioni 64 kitakapoanza kutumika.

LIVE IN PLAY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 823

MECHI KALI

REAL MADRID
VERSUS
VALENCIA

1 | 1.41
X | 4.81
2 | 7.04

PIGA *150*87#


Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ

HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# DEST KUMRITHI TRIPPIER ATLETICO




**LONDON,** England

KLABU ya Atletico Madrid inaweza kumgeukia nyota wa Barcelona, Sergino Dest wakati Kieran Trippier akitarajiwa kuondoka.

Ripoti zinataja Trippier anaelekea kuondoka Atletico Madrid baada ya kuwapo kwa zaidi ya miaka miwili na kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, msimu uliopita.

Newcastle United wanatarajiwa kukamilisha usajili wa beki huyo wa kulia ndani ya siku moja au mbili zijazo.

Na hiyo itawaacha Atletico Madrid wakiwa na upungufu katika nafasi ya beki ya kulia, huku Sime Vrsaljko akiwa hana uwezekano wa kuchukuliwa kama chaguo la kwanza.

Dest ameshindwa kufanya vizuri chini ya kocha Xavi Hernandez, na amekuwa akihusishwa na kutaka kuondoka Barca.

Xavi ameweka wazi Dest angeshiriki zaidi kama hangepata jeraha, huku ESPN ikiripoti kuwa raia huyo wa Marekani anatamani sana kubakia pale Camp Nou.

Lakini pia inaripotiwa Atletico Madrid wanamwona Dest kama mbadala mzuri wa Trippier na hiyo inaweza kuwa hali ya kuvutia uhamisho.

## *Fiorentina wanogewa na Torreira*

**LONDON,** England

MKURUGENZI wa Soka wa Fiorentina, Daniele Prade amethibitisha timu hiyo ya Ligi Kuu Italia, Serie A, imekaa na Arsenal kujadili uhamisho wa kudumu wa Lucas Torreira.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uruguay alipata changamoto kurejea katika kikosi cha Arsenal chini ya Mikel Arteta na pia alivumilia msimu uliopita wa mkopo akiwa na Atletico Madrid.

Kurejea Amerika Kusini ilikuwa ni pendekezo kwa Torreira baada ya kifo cha mama yake, lakini tangu wakati huo aliwekeza nguvu kubakia Fiorentina.

Prade sasa amebainisha mazungumzo juu ya uhamisho wa kudumu yatafanyika hivi karibuni.


"Tumefurahishwa na Lucas, lakini bado hatuwezi kuzungumza chochote kwa sasa. Tutazungumza Machi au Aprili na Arsenal, klabu ambayo tuna uhusiano nayo mkubwa."

Torreira anajivunia mabao manne na asisti sita katika mechi 89 alizochezea Arsenal na ameanza mechi 14 za Serie A akiwa na Fiorentina msimu huu.



## HABARI MICHEZO

,998,440



# NYOTA TEMBO WARRIORS ANG'AA, ATAKIWA UTURUKI

**Na Saada Akida**

MCHEZAJI wa Timu ya Soka ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu (Tembo Warriors), Frank Ngailo, amepokea ofa ya kwenda kujiunga na klabu ya Izmir BBSK ya nchini Uturuki, imefahamika.

**Ngailo amepata ofa hiyo baada ya kuchaguliwa kuwa Mchezaji Bora katika mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (CANAF 2021) yaliyofanyika hapa nchini mwaka jana.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Watu wenye Ulemavu (TAFF), Peter Sarungi, alisema ataenda kufanya majaribio lakini alikiri kufanya vyema katika michuano ya CANAF kulimsaidia mchezaji huyo kupata nafasi.


Sarungi alisema ni heshima kwa Tanzania na nyota huyo binafsi kupata nafasi ya kwenda kucheza soka la kulipwa na anaamini itaongeza chachu na kufungua milango kwa wachezaji wengine wa hapa nchini.

"Viongozi tutapambana kuhakikisha Ngailo anafanikisha safari yake, kwa sababu tunahitaji kuona hatupotezi nafasi hiyo ambayo ni muhimu kwa Taifa. Ni fahari na heshima kwa TAFF na Tanzania kwa ujumla ni chachu kwa wachezaji wengine kuongeza bidii hasa kipindi hiki tunachojiandaa kucheza Kombe la Dunia," alisema Sarungi.

Aliongeza wanatarajia nyota huyo atajiimarisha na kupata uzoefu zaidi ambao utaisaidia Tembo Warriors katika kufanya vyema kwenye michuano ya Kombe la Dunia itakayofanyika baadaye mwaka huu.

"Naamini ndoto zetu zinaendelea kutimia, kupata nafasi ya kwenda kwenye majaribio ni faraja kwetu, ninaamini atafanya vyema na kuchukuliwa rasmi na hao Waturuki," Sarungi alisema.

Fainali za Kombe la Dunia kwa Watu wenye Ulemavu zinatarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu nchini Uturuki na Afrika itawakilishwa na Tanzania, Misri, Liberia na Morocco.




Kocha Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkomwa (kushoto), akisalimiana na Kocha wa Yanga Princess, Edna Lema kabla ya kuzungumzia mechi ya 'dabi' ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# *Coastal kusajili mastraika wapya*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Melis Medo, amesema akili na nguvu zake zinaelekea katika kuimarisha safu ya ushambuliaji ili kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kupata matokeo chanya katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo itaendelea tena kuanzia wiki ijayo.

Melo aliliambia gazeti hili licha ya kuwaamini wachezaji waliopo, lakini anahitaji kuboresha kikosi chake kulingana na mahitaji halisi na ushindani uliopo kwenye ligi hiyo.

"Nimejiandaa kufanya maboresho katika kikosi chetu, hasa tutaangalia safu ya ushambuliaji, inahitaji kuimarishwa zaidi," alisema Medo.

Kocha huyo alisema malengo yake ni kuyafanyia kazi mapungufu yote aliyoyabaini wakati huu wa dirisha dogo ili wajiweke kwenye nafasi nzuri ya kumaliza msimu katika nafasi za juu.

"Ligi imekuwa na ushindani mkubwa, kila timu imefanya usajili na kutumia kipindi hiki cha usajili kuboresha na kufanyia kazi mapungufu, pia kwetu tumeona madhaifu yetu, tunayafanyia kazi kwa kuboresha kila nafasi," alisema Medo.

Katika msimamo wa Ligi Kuu ya NBC Tanzania Bara, Coastal Union yenye pointi 17 inashika nafasi ya nne baada ya kushinda michezo minne na kutoka sare mara tano huku ikifungwa michezo miwili.


## JACKPOT
### MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. 9/1/22 | 16:30 | Cagliari vs Bologna | 3.15 | 3.30 | 2.27 |
| 2. 9/1/22 | 16:30 | Torino vs Fiorentina | 2.56 | 3.41 | 2.66 |
| 3. 9/1/22 | 17:00 | Clermont Foot vs Reims | 2.42 | 3.14 | 2.99 |
| 4. 9/1/22 | 17:30 | Hertha BSC vs FC Koln | 2.66 | 3.46 | 2.51 |
| 5. 9/1/22 | 19:05 | Nantes vs Monaco | 3.22 | 3.27 | 2.23 |
| 6. 9/1/22 | 20:15 | Malaga vs Sporting Gijon | 2.43 | 3.04 | 2.95 |
| 7. 9/1/22 | 20:30 | Alaves vs Athletic Bilbao | 3.25 | 3.05 | 2.35 |
| 8. 9/1/22 | 20:30 | Roma vs Juventus | 3.07 | 3.31 | 2.31 |
| 9. 9/1/22 | 20:30 | Genoa vs Spezia | 2.28 | 3.29 | 3.14 |
| 10. 9/1/22 | 22:30 | Ponferradina vs Zaragoza | 2.43 | 3.04 | 2.95 |
| 11. 9/1/22 | 23:00 | Villarreal vs Atletico Madrid | 2.84 | 3.19 | 2.54 |
| 12. 9/1/22 | 23:30 | Las Palmas UD vs Almeria | 2.76 | 3.05 | 2.56 |
| 13. 9/1/22 | 23:30 | Belenenses vs FC Arouca | 2.57 | 3.02 | 2.82 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 08/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:15 | 3608 | Mansfield vs Middlesbrough | 5.14 | 3.85 | 1.61 |
| 15:30 | 2743 | Hartlepool vs Blackpool | 4.44 | 3.65 | 1.74 |
| 15:30 | 3977 | Coventry vs Derby | 1.81 | 3.64 | 4.03 |
| 15:30 | 4039 | Bristol City vs Fulham | 4.54 | 3.75 | 1.70 |
| 15:30 | 5930 | Burnley vs Huddersfield | 1.68 | 3.84 | 4.53 |
| 15:45 | 1300 | Millwall vs Crystal Palace | 3.30 | 3.40 | 2.09 |
| 16:00 | 1093 | Alanyaspor vs Basaksehir | 2.73 | 3.27 | 2.48 |
| 16:00 | 2172 | Levante vs Mallorca | 2.18 | 3.30 | 3.35 |
| 17:00 | 1042 | Le Havre vs Sochaux | 2.46 | 3.10 | 2.85 |
| 17:30 | 1895 | Bayer Leverkusen vs Union Berlin | 1.82 | 3.79 | 3.99 |
| 17:30 | 3572 | Hoffenheim vs Augsburg | 1.56 | 4.36 | 5.16 |
| 17:30 | 4231 | SC Freiburg vs Arminia Bielefeld | 1.60 | 3.93 | 5.37 |
| 17:30 | 4368 | RB Leipzig vs Mainz | 1.77 | 3.84 | 4.19 |
| 17:30 | 5893 | Greuther Furth vs Stuttgart | 3.53 | 3.58 | 1.99 |
| 18:00 | 1485 | Wigan vs Blackburn | 2.80 | 3.30 | 2.41 |
| 18:00 | 1678 | West Bromwich vs Brighton | 3.11 | 3.36 | 2.19 |
| 18:00 | 1850 | Ayr United vs Arbroath | 3.66 | 3.32 | 1.96 |
| 18:00 | 2307 | Inverness vs Raith Rovers | 2.28 | 3.17 | 3.03 |
| 18:00 | 2362 | Newcastle vs Cambridge Utd | 1.25 | 5.51 | 10.81 |
| 18:00 | 2770 | FC Cartagena vs Huesca | 2.35 | 3.05 | 3.05 |
| 18:00 | 2944 | Hamilton vs Partick Thisle | 2.88 | 3.23 | 2.34 |
| 18:00 | 4120 | Port Vale vs Brentford | 7.52 | 4.65 | 1.38 |
| 18:00 | 4904 | Kidderminster vs Reading | 5.53 | 3.95 | 1.56 |
| 18:00 | 5035 | Peterborough vs Bristol Rovers | 1.39 | 4.54 | 7.31 |
| 18:00 | 5296 | QPR vs Rotherham | 1.99 | 3.45 | 3.54 |
| 18:00 | 5372 | UD Ibiza Eivissa vs Alcorcon | 1.91 | 3.19 | 4.13 |
| 18:00 | 5618 | Boreham Wood vs AFC Wimbledon | 3.31 | 3.41 | 2.09 |
| 18:00 | 5647 | Barnsley vs Barrow | 1.47 | 4.24 | 6.31 |
| 18:00 | 5669 | Leicester vs Watford | 1.57 | 4.14 | 5.12 |
| 18:15 | 2487 | Real Sociedad vs Celta Vigo | 1.84 | 3.46 | 4.41 |
| 18:30 | 2268 | FC Vizela vs Moreirense | 2.36 | 3.12 | 3.02 |
| 19:00 | 4871 | Galatasaray vs Giresunspor | 1.61 | 3.85 | 5.14 |
| 20:15 | 5075 | Valladolid vs Burgos | 1.54 | 3.89 | 5.71 |
| 20:30 | 1546 | Hull City vs Everton | 3.56 | 3.51 | 1.97 |
| 20:30 | 1726 | Chelsea vs Chesterfield | 1.03 | 12.79 | 34.44 |
| 20:30 | 2657 | Swansea vs Southampton | 3.32 | 3.42 | 2.08 |
| 20:30 | 2858 | Granada vs Barcelona | 4.13 | 3.65 | 1.84 |
| 20:30 | 3647 | Eintracht Frankfurt vs Borussia Dortmund | 3.33 | 3.98 | 1.95 |
| 20:30 | 4808 | Birmingham vs Plymouth | 1.98 | 3.45 | 3.55 |
| 20:45 | 4540 | Yeovil vs Bournemouth | 7.69 | 4.64 | 1.37 |
| 21:00 | 1608 | Bastia vs US Quevilly Rouen | 1.88 | 3.33 | 4.02 |
| 21:00 | 2051 | PAU FC vs Rodez Aveyron | 1.88 | 3.28 | 4.11 |
| 21:00 | 4274 | GD Estoril vs Porto | 29.62 | 9.68 | 1.07 |
| 21:00 | 4516 | Dijon vs Nimes | 2.12 | 3.34 | 3.24 |
| 21:00 | 5701 | Grenoble Foot vs AJ Auxerre | 2.85 | 3.10 | 2.46 |
| 21:00 | 5724 | Valenciennes vs Guingamp | 2.77 | 3.11 | 2.52 |
| 23:00 | 1238 | Real Madrid vs Valencia | 1.41 | 4.81 | 7.04 |
| 23:00 | 5074 | Lens vs Rennes | 2.74 | 3.38 | 2.48 |
| 23:00 | 5400 | Leganes vs Real Sociedad B | 1.76 | 3.15 | 5.12 |
| 23:30 | 2177 | Boavista vs Tondela | 1.99 | 3.35 | 3.65 |

# Michezo

Jumamosi Januari 8, 2022

Nipashe




Mbio kumnasa Haaland zakolea UKURASA 21



Kiungo wa Yanga, Feisal Salum 'Fei Toto' (kulia), akijiandaa kumtoka mchezaji wa KMKM katika mechi ya mashindano ya Kombe la Mapinduzi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar jana. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: MTANDAO**

## Watani wanawake kumaliza ubishi

**Na Saada Akida**

NI 'dabi' ya kusaka heshima na kulipiza kisasi ambapo Yanga Princess inatarajiwa kuwakaribisha Simba Queens katika mechi ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itakayochezwa leo kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza jijini jana, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, alisema kikosi chake kimejiandaa vizuri kuelekea katika mechi hiyo na wanatarajia kuondoka na pointi tatu muhimu.

Edna alisema anaiheshimu Simba Queens kwa sababu ni timu bora na imefanya usajili mzuri msimu huu, hivyo wataingia uwanjani kwa tahadhari ili kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kupata matokeo chanya katika mchezo huo.

"Hakuna majeruhi katika kikosi changu, wachezaji wote wako fiti na tayari kwa mchezo huo, tutahakikisha tunacheza kwa tahadhari kubwa na kutorudia makosa ya nyuma kwa kuangalia udhaifu wa Simba Queens ili kupata ushindi," alisema Edna.

Nahodha wa Yanga Princess, Fatma Mwisendi, alisema wanawaheshimu wapinzani wao na kwa sababu hiyo watacheza kwa kufuata maelekezo na mbinu kutoka kwa benchi lao la ufundi.

"Ni mechi ya ushindani, tunahitaji zaidi matokeo tunaenda kupambana kwa sababu Simba Queens wametuzidi pointi mbili ambazo tunahitaji kuzipata kwao na kuwashusha kileleni walipokuwapo sasa," alisema Fatma.

Naye Kocha wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, alisema wachezaji wake wote wako fiti na wako tayari kuendelea pale walipoishia.

"Tunatarajia kwenda kutafuta matokeo chanya, suala la idadi kubwa ya mabao ambayo tulikuwa tukiyapata mechi zilizopita siwezi kusema kwa sababu hakuna 'dabi' rahisi, tutaingia kupambana kusaka matokeo mazuri," alisema Violeth Nicholas, nahodha wa Simba Queens.

# Yanga, Azam nusu fainali

## ●●● Yalazimishwa sare na KMKM katika...

**Na Faustine Feliciane**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la Mapinduzi, Yanga imefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo baada ya kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya KMKM katika mechi ya mwisho ya Kundi B iliyochezwa kwenye Uwanja wa Amaan, Zanzibar jana.

**Yanga imesonga mbele baada ya kuongoza kundi hilo ikiwa na pointi nne sawa na KMKM, lakini mabingwa hao watetezi wana faida ya uwiano mzuri wa mabao ya kufunga ukilinganisha na wenyeji KMKM.**

Timu hizo mbili zote zilipata ushindi zilipokutana na Taifa Jang'ombe, ambapo Yanga ilishinda mabao 2-0 wakati KMKM iliwachapa 'ndugu' zao magoli 2-1.

KMKM iliuanza mchezo huo kwa kasi wakiwabana vilivyo Yanga karibu dakika zote za kipindi cha kwanza huku pia wakifanya mashambulizi zaidi kupitia katikati ya uwanja lakini makosa ya mlinzi wa kulia wa 'Maafande' hao kilizawadia Yanga bao la kuongoza sekunde chache kabla ya mapumziko kupitia kwa mshambuliaji, Heritier Makambo.

Kiungo wa Yanga, Dickson Ambundo alimzidi ujanja beki wa pembeni wa KMKM na kumpokonya mpira kabla ya kupiga krosi iliyomkuta Makambo na kuunganisha kwa kichwa.

Mpaka timu hizo zinaenda mapumziko, Yanga walikuwa mbele kwa bao moja, lakini waliingia kipindi cha pili kwa mabadiliko ya kumtoa Dennis Nkane ambaye jana alionekana kuwa na wakati mgumu mbele ya mabeki wa KMKM na kuingia, Jesus Moloko huku pia wakiwatoa Ambundo na Yassin Mustafa na nafasi zao kuchukuliwa na David Bryson na Farid Mussa.

Dakika ya 54, KMKM walisawazisha bao hilo kupitia kwa Abrahman Ali aliyeunganisha kwa kichwa mpira wa adhabu.

Bao hilo liliwafanya Yanga kuongeza kasi na kufanikiwa kupata bao la pili kupitia kwa Feisal Salum 'Fei Toto' ambaye alitumia makosa ya mabeki wa KMKM kuzembea mpira kumkaba Makambo ambaye alitoa pasi fupi kwa mfungaji huyo aliyeachia shuti kali lililotinga wavuni moja kwa moja.

Wakati Yanga wakiamini wanaondoka na pointi zote tatu kwenye mchezo huo, mshambuliaji, Hamad Abdalla Juma aliwashangaza kwa kufunga bao la kusawazisha baada ya kuuwahi mpira wa adhabu ndogo uliopigwa haraka haraka na kumchambua kipa wa Yanga, Aboutwalib Mshery na kufanya dakika 90 kumalizika kwa kugawana pointi.

Timu nyingine iliyotinga hatua ya nusu fainali ni Namungo FC ambayo inasubiri timu itakayomaliza kinara katika Kundi C ambayo ni Simba au Mlandege.

Mechi za hatua ya makundi zitamalizika leo kwa Azam FC kuivaa Yosso Boys, mchezo ambao ni wa kukamilisha ratiba kufuatia klabu hiyo ya Pemba kupoteza mechi zake mbili za awali zilizotangulia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >